ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Saba – Tarehe 27 Januari, 2011

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 71

Utengenezaji wa Barabara kwa Kutumia Vifaa Duni

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad - Aliuliza:-

Kwa kuwa utengenezaji wa bara bara ya Chambani ikiwa ni pamoja na kung'oa miti, kukata milima umekuwa ukitumia teknolojia duni ya kutegemea nguvu kazi watu, majembe ya mkono, masururu, mapanga na mapauro.

(a) Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo ni aibu kwa karne hii na inaathiri afya za wananchi na kupelekea kuendelea kuishi katika hali ngumu ya maisha.

(b) Kwa utaratibu huu wa kutumia teknolojia duni, Je, Serikali haioni kuwa kukamilika kwa matengenezo ya barabara hiyo kutachukua muda mkubwa kinyume na ilivyokusudiwa.

(c) Kwa kuwa barabara hii haitopita maeneo ya Chambani ambako kuna wakaazi wengi. Je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha huduma hii kuanzia vijiji vya Waami, Tondooni, Kekewani, Chwale, Matale hadi Ukutini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 71 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kabla ya kujibu vifungu vya suala husika naomba kutoa maelezo mafupi yanayohusiana na njia inayotumika katika ujenzi wa Mradi wa Barabara za Ndani – Kusini Pemba ambazo pamoja na barabara nyengine unajumuisha barabara ya Kenya – Chambani.

Mhe. Spika, mradi nilioutaja unahusisha ujenzi wa barabara za ndani zenye jumla ya kilomita 43.7 zifuatazo:

(i)	Chanjamjawiri – Tundauwa,	11km;
(ii)	Chanjaani – Pujini,	5km;
(iii)	Mzingani – Wambaa,	9.7km;
(iv)	Kenya – Chambani,	3.2km;
(v)	Mtambile – Kangani,	6.4km;
(vi)	Mtambile – Mwambe,	9.4km.

Mradi huu unafadhiliwa na Nchi ya Norway, kusimamiwa na kampuni ya *POYRY* kutoka Switzerland na kutekelezwa na Idara ya Barabara kwa mfumo unaojumuisha matumizi ya Wafanyakazi na Mashine. Mfumo huu unafaida nyingi katika utekelezaji wake kwa barabara ndogo ndogo ukilinganishwa na njia za matumizi ya mashine *(mashine intensive method)* ambazo tumezizowea.

Katika ujenzi wa barabara husika, shughuli za utengezaji mitaro, ujenzi wa mabomba, usambazaji kifusi kikavu, kifusi kilochanganywa na lami *(emulsion treated base, ETB),* la lami baridi *(cold asphalt*) shughuli hizi zote hufanywa na wafanyakazi, na zile zilizobaki hufanywa na mashine ambazo hujumuisha un'goaji miti, usafishaji njia na ukataji milima, uchimbaji na upakizi wa kifusi, usafirishaji wa kifusi na vifaa hufanywa na mashine.

Ujenzi wa barabara kwa mfumo huu ni mpya na umetumika kwa mafanikio nchini Afrika ya Kusini, Kenya na kwengineko duniani. Njia hii ya ujenzi sio 'teknologia duni' bali ni mfumo unaoonekana sasa kuwa ni ufumbuzi wa matatizo ya upatikanaji wa huduma za barabara vijijini. Miongoni mwa faida nyingi za mfumo huu wa ujenzi ambazo tumezipata katika mradi wetu huu ni:

i. Ujenzi huu una gharama ndogo ukilinganishwa na ule wa utumiaji mashine. Barabara tunazozijenga zinagharimu kati ya shilingi milioni 140 – 250 kwa kilomita wakati kwa kutumia mashine zingegharimu shilingi milioni 850 – bilioni 1.2. kilomita moja pale tunapotumia mashine peke yake.

ii. Mradi umetengeneza ajira kubwa kwa wananchi ambapo hadi kufikia mwisho wa mwaka 2010, jumla ya wananchi 960 walipatiwa ajira ambapo kiasi cha shilingi 509,281,500 zililipwa kwa wananchi na wafanyakazi hao. Hadi kukamilika kwa mradi imekisiwa malipo hayo yatakuwa ni shilingi bilioni moja itakuwaq imelipwa kwa wafanyakazi hao.

iii. Ushiriki wa wananchi unasaidia kuwapa mafunzo ya kazi za ujenzi na utunzaji wa barabara na hivyo kuwa na kujiajiri katika shughuli za utunzaji wa barabara hizo mara zitakapokamilika. Hivi sasa Wizara yetu inatekeleza shughuli nyingi za utunzaji wa barabara kwa kutumia wakandarasi na vikundi binafsi kwa mikataba.

iv. Mfumo huu umevutia taasisi za elimu ya juu kutuma wanafunzi wao kuja kujifunza kuchukua technologie hiii. Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kujibu suala la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mwakilishi kuwa hatuna sababu ya kuona aibu kwa kutumika mfumo huu. Kwani mfumo huu ni wa kitaalam unajenga barabara madhubuti na kwa gharama nafuu sana kama tulivyoeleza hapo awali. Aidha ujenzi huo unashirikisha jamii maeneo husika huku suala la afya za watendaji kazi na mazingira yakipewa kipaumbele.

(b) Mradi huu umepangwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu 2011. Hivi sasa ujenzi wa barabara nne kati ya sita zilizomo katika mradi huu unaendelea sambamba. Hatua za ujenzi zimefikia katika viwango vifuatavyo:

- Barabara ya Mtambile – Mwambe (9.4km): Kazi zote zimekamilika imebaki uwekaji lami kwa kilomita 6 tu kilomita tatu zimeshafanywa.

- Barabara ya Mtambile – Kangani (6.4km): Hivi sasa tunakamilisha uwekaji wa *'base'* na kazi za uwekaji lami zitaanza karibuni.

- Barabara ya Mzingani – Wambaa (9.7km): Kazi za usafishaji, ujenzi wa mitaro na mabomba ya kupitisha maji umefikia kilomita 8. Kazi zinaendelea kama zilivyopangwa.

- Barabara ya Kenya – Chambani (3.2km): Usafishaji na ujenzi wa mabomba umekamilika kwa urefu wa kilomita 1.5

Kazi zote zilizobaki katika barabara hii na zile za Chanjamjawiri – Tundauwa na Chanjaani – Pujini zitakamilishwa kwa wakati.

(c) Ni kweli kuwa vijiji vya Waami, Tondooni, Kekewani, Chwale, Matale na Ukutini havitapitiwa na barabara ya Kenya – Chambani ambayo imo katika mradi huu. Napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mwakilishi kuwa, vijiji hivyo vitaunganishwa kwa kupitiwa na barabara tunayotaraji kuijenga itokayo Ole hadi Kengeja. Barabara hii itaungana na barabara inayojengwa hivi sasa ya Kenya – Chambani.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, pamojana majibu mazuri na marefu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri pamoja na kueleza kwamba wananchi miongoni mwa shirikishi yao ni kupata ajira, lakini Mhe. Waziri jua kwamba ajira hii ambayo wanalipwa wananchi hawa ni duni ambayo haikamilishi mahitaji yao ya kila siku, na wakati huu wanatumia kwa kuchonga milima kutengenezwa barabara hii ndio wakati ambao wangeutumia kwa ajili ya kilimo ambao ndio kazi yao ya msingi.

a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kuwaajiri watu hawa kutengeneza barabara kwa malipo duni ni kuwarudisha nyuma katika maisha yao ya kilimo walichokizoea.

b) Barabara ambayo itajengwa na kuwashirikisha wananchi hao wa Kekewani, Tondooni na Matele inatarajiwa kujengwa muda gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miungombinu: Nadhani Baraza hili litakubaliana nami suala la ajira ni suala la hiari, utaratibu uliotumika katika kuwaajiri watu hawa ulikuwa ni utaratibu wa hiyari wao wenyewe walileta maombi Wizara ilitafuta utaratibu mzuri wa kutowanyima fursa ya kuwapatia, tunaamini walijitokeza kwa hamasa na hamu ya kuona na wao wanatoa nguvu zao katika kujenga taifa lao.

Siamini kwamba kipato wanacholipwa ni kipato duni kama Mhe. Mwakilishi anavyosema, watu hawa wanalipwa Shs. 150,000 mpaka 160,000 kwa mwezi, naamini kipato hiki sio kidogo kama anavyosema kwani kiwango chetu cha

mwisho cha mshahara ni Shs. 100,000/= kwa sheria zetu naamini kiwango hichi sio duni.

Lakini suala la pili barabara hii kama majibu yetu ya awali tuliyosema kwamba tunataraji baada ya kukamilisha mchakato kupata mkandarasi, barabara hii itaanza kujengwa kwani wafadhili wameshatupatia fedha hizo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Miongoni mwa barabara ambazo amezitaja ni barabara ya Mtambili/Mwambe yenye urafu wa k.m 9.4 km
Watu wa Pemba wamezoea kila ambapo barabara hujengwa Pemba zana za kujenga kama kokoto hutoka Mwambe, Micheweni ama Vitongoji. Lakini barabara hizi sita tumeshuhudia kokoto kutoka Kenya.

a) Je, ni sababu zipi ambazo wizara imeona sasa iagizie kokoto kutoka Kenya badala ya kuchukua kokoto kutoka Mwambe, Vitongoji au Micheweni.

b) Kilomita 3 ambazo zimetiwa lami barabara ya Mtambile/Mwambe kila ambapo ng'ombe anaweka kinyesi barabara ile inabomoka na kuondoka pande la ardhi. Je, ni kwa nini kinyesi cha ng'ombe kimekuwa ni rahisi kubomoa barabara zile ni sumu au kiwango duni cha barabara.

c) Kwenye ujenzi wa barabara hizo wananchi wengi wameathirika kwa vipando na nyumba, ni lini wizara itawalipia wananchi wa Mtambile/Mwambe fidia vipande vyao ambavyo vimeharibiwa kwa ujenzi wa barabara hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Kwanza napenda nimthibitishie kwamba mradi huu ni mpya kwetu kama majibu mama tulivyoyasema, upya huo ndio uliopelekea kuchukua kokoto Kenya katika kuona namna ya kufanya mradi huu ukamilike vizuri, kwa maana kwenye utafiti wetu utatupa majibu kiasi gani.

Suala la pili niseme sikubaliani nae kusema kinyesi cha ng'ombe kinasababisha uharibifu wa barabara, lakini pia napenda kumhakikishia Mhe. Mwekilishi kwamba tuko tayari wizara yetu kushirikiana na taasisi husika kwenda kufanya utafiti kuhusiana na malalamiko haya aliyoyaleta Mhe, Mwakilishi.

Lakini suala la tatu Wizara yetu kwa kushirikiana na serikali tutahakikisha pale tutakapopatiwa fedha mradi huu wa kuwalipa watu fidia tunaukamilisha kama tulivyoahidi awali.

Nam. 74

Viwanja vya Zanzibar Kubadilishwa Majina

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliulzia:-

Hivi karibuni Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar kimebadilishwa jina na kuitwa "*Abeid Amani Karume International Airport"* na Kiwanja cha Pemba kubakia na jina lile lile la Pemba Airport, na suala (b) lisijibiwe.

(a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar kubadilishwa jina.

(b) Kwa kuwa miongoni mwa majina makubwa na yenye historia muhimu kwa uhuru wa Zanzibar ni pamoja na Mzee Thabit Kombo, kwa nini kiwanja cha Pemba hakipewi jina la kiongozi huyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 lenye vifungu (a), (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Kiwanja cha ndege cha Zanzibar kimebadilishwa jina na kuitwa *Abeid Amani Karume International Airport* ili kulitukuza na kulienzi jina la Muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 na Rais wa Kwanza wa Visiwa vya Unguja na Pemba, serikali imependekeza jina hilo baada ya kuongezeka kwa hadhi ya uwanja wetu wa ndege samba na heshima kubwa aliyokuwa nayo muasisi huyo wa nchi yetu, aidha utaratibu kama huu unatumika sehemu nyingi duniani mfano Dar es Salaam unaita Mwalimu Nyerere International Air Port, wenzetu wa Kenya Uwanja wa Naiorobi wanaita Jomo Kinyata na Mombaza wanaita Moi International Air Port.

(b) Mhe. Spika, hivi sasa Serikali haijafikiria jina hilo la Kiwanja cha Ndege cha Pemba kuitwa Kiwanja cha Ndege cha Thabit Kombo lakini hata hivyo Wizara yangu italifikiria suala hilo baada ya kufanywa marekebisho na maboresho makubwa ya uwenja wetu wa ndege wa Pemba.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b kwa pamoja

Amesema kwamba sababu kubwa ya kubadilisha jina kiwancha cha ndege cha Zanzibar ni kutokana na hadhi ya kiongozi wetu kwamba ndio mkombozi wa Zanzibar, sasa kwa misingi hiyo hiyo ya hazi ya kiongozi wetu. Yapo malalamiko kwamba hivi karibuni wakati ndege inajiandaa kutua kilwanja kile kilikuwa na mbwa wengi ndani.

a) Je, hali hiyo ndio inalingana na hadhi ya kiongozi wetu na sifa za kimataifa ndio zinakamilia.

b) Pembezoni mwa kiwanja hicho zipo ndege za kampuni ya INDIGO naomba kujua ndege zile zilipo ni gereji au zimekaa kwa sababu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu:

a) utaratibu wa ujenzi kwa maana ua uzio wa kuzungurusha uwanja wetu hivi sasa umefikia hatua nzuri na siamini kwamba tena kutakuwa na sababu au sehemu ya mbwa kupita kuingia kwenye uwanja, tumeboresha uwanja wetu na hivi sasa upo katika hatua nzuri na nahakikisha kwamba hata hatua za kiusalama tumeongeza kampuni ambayo tumeiajiri kufanya shughuli hizo za kukinga mpya na hata binaadam.

b) Ni kweli zipo ndege ambapo kimaumbile tunajua kwamba ndege inaondoka kwenye uwanja wa ndege hadi kwenye uwanja wa ndege, hakuna sehemu nyengine ya kukaa ndege na ndege zile ziko pale kwa kusubiri utaratibu wa matengenezo na kuondoka kwenda sehemu nyengine, tumefanya mawasiliano kuwasiliana na wenyewe kuweza kuona kwa muda gani watakaa pale ili kuweza kutoa nafasi kwa shughuli nyengine za matumizi ya uwanja wa ndege.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, pajama majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kumekuwa na uharibifu mkubwa kutokana na uchimbaji wamchanga pembezoni mwa uzio wa kiwanja cha ndege cha Zanzibar.

a) Je, wizara hii imechukua hatua gani juu ya suala hili.

b) Je, Wizara haioni kuwa na haja ya kuweka walinzi pembezoni mwa kiwanja hicho ili kunusuru mandhari ya kiwanja chetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Wakati namjibu Mhe. Hija nilisema kwamba tumeajiri kampuni kwa ajili ya kufanya ulinzi kwa maeneo yetu ya uwanja wa ndege. Napenda kumuhakikishia Mheshimiwa Wizara yetu kwa kushirikiana na vikosi vya ulinzi na usalama pamoja na taasisi husika tumepiga marufuku shughuli za uchimbaji wa mchanga hasa maeneo ya mashariki ya uwanja wetu wa ndege.

Mhe. Subati Khami Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa sababu katika bandari zote meli zinapotia nanga na zikawa zimekaa siku nyingi hazijaondoka kila siku moja inagharamia kulipa eneo la bandari kwa ajili ya kukaa kwenye bandari ile.

Je, Mhe. Waziri ndege zile zilizokaa pale na siku nyingi kama hizo kuna malipo yoyote yanayofidia uwanja wetu kwa ndege zile.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Katika majibu yangu niliyomjibu Mhe. Hija nilisema kwamba wizara yetu kwa kupitia mamlaka ya kiwanja cha ndege tunafanya mawasiliano na wamiliki wa ndege ile, aidha katika mawasiliano yale tutaona utaratibu na sheria zinazoongoza viwanja vya ndege zinasemaje, ikiwa kuna utaratibu wa kulipa malipo tutataka Idara husika kwa maana ya kwamba wenye ndege wawasiliane na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege waweze kutulipa fidia hiyo kama taratibu zinaruhusu.

Nam. 40

Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-

Imekuwa ni mazoea kwa viongozi na wananchi wa Zanzibar kukiita Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar kuwa ni cha Kimataifa.

(a) Je, Mhe. Waziri ni sifa zipi zinakifanya kiwanja hicho kuitwa cha Kimataifa.

(b) Je, kiwanja chetu cha Zanzibar kinatosheleza sifa hizo.

(c) Kama hakitoshelezi, kwa nini kiitwe cha Kimataifa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 40 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwekilishi suali lake na 40 naomba kutoa tafsiri halisi ya neno Kiwanja cha ndege cha Kimataifa kama ilivyoelezwa na jumuiya ya Kimataifa, kuhusiana na masuala ya usafiri wa Anga duniani.

Mhe. Spika, kiwanja cha ndege cha kimataifa ni kwanja ambacho nchi husika hukiteua kutumia ndege za kimataifa pamoja na huduma nyengine za msingi kma vile Forodha, ambapo huduma za msingi huwa zinapatikana huduma ambazo ni kama Forodha, Uhamiaji, Huruma za Afya na nyenginezo, viwanja vya ndege vya aina hii aghalabu huwa ni vikubwa na vyenye barabara za kurukia na kutulia ndege zenye urefu wa kutosha pamoja na hoduma nyengine muhimu kwa ajili ya kuhudumia abiria na ndege za mizigo katika viwanja hivyo.

Aidha mbali na kuhdumia ndege za kimataifa viwanja hivi pia huweza kuhudumia ndege za ndani kwa maana ya *domestic flyt* na kuwa na safari nyingi za mashirika ya ndege ya kigeni, abiria wanaosafiri katika viwanja hivi hutakiwa kufuata taratibu zote za usafiri na usalama kama vile uhamiaji, pamoja na Forodha wakati wa kuingia na kutoka nchini.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake kama hivi ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Zanzibar ambacho hivi sasa kinajulikana kwa jina la Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume pamoja na huduma nyengine una huduma za msingi za uhamiaji, afya na masuala la forofha kwa ajili ya kuhudumia ndege ambao kwa ujumla wake ndizo zinazofanya kuitwa Uwanja wa

ndege wa Kimataifa. Mbali na huduma hizo za msingi uwanja huu una huduma zifuatazo kwa ajili ya kuhudumia ndege za kimataifa.

(i) Barabara ya kutulia na kurukia ndege ni refu na yenye uwezo wa kutosha.

(ii) Vijia kwa ajili ya ndege kuweza kuelekea kwenye maegesho vipo vya kutosha.

(iii) Eneo la maegesho lipo la kutosha kwa ndege zote zinazokuja.

(iv) Uimara wa barabara ya kutulia na kurukia ndege, vijia vidogo pamoja na eneo la maegesho yapo ya kutosha.

(v) Huduma za Zimamoto na Uokozi katika Kiwanja kwa kiwango stahiki zipo kama viwango vinavyoelekeza. *(ICAO category).*

(vi) Kuweko kwa huduma za mafuta ya ndege pamoja na ndege zenyewe zipo.

(vii) Mitambo ya kuongozea ndege pamoja na taa za kusaidia ndege kutua wakati wowote usiku na mchana ipo.

Mhe. Spika, jibu b na c ni kwamba baada ya kuangalia sifa hizo zote kiwanja chetu cha Abeid Amaan Karume kinastahiki na kina hizi sifa za kuitwa kiwanja cha kimataifa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu a, b na c.

Kwa kuwa hiki ni kiwanja cha kimataifa yaani *International Air Port* viwanja vingi vya kimataifa tulivyopata taarifa duniani duniani zimamoto ni sehemu ya kile kiwanja na haipo katika Zimamoto ya nchi.

(a) Ni sababu zipi mpaka leo kwamba Zimamoto ya kiwanja chetu cha kimataifa ikawa haijawa ni sehemu moja ya kile kiwanja yaani utawala wake ukatoka pale pale.

(b) Kwa sababu kinahudumia kimataifa na kitaifa, habari ya wengi huwa wanataka kusikia matangazo yanayotoka katika kipaza sauti, kwa sababu inawezekana kwamba mtu amekwenda chooni na ndege iko

tayari. Je ni sababu zipi kiwanja hichi cha Kimataifa ikawa mpaka leo ikawa hakina kipaza sauti.

(c) Viwanja vingi kwa wale wanaosafiri wataniunga mkono, unamopita huwa kuna bodi ya matangazo huonesha ndege zinazotua na kuondoka. Lakini kiwanja chetu hakina katika teknolojia hii ya *electronic volume*. Je, ni sababu zipi kiwanja chetu kikawa hakina hicho na zipo bodi ndogo na kubwa kutokana na viwanja vyetu. Yaani kutokana na kiwanja ukubwa wake kilivyo. Unaweza ukanunua bodi ya matangazo ndogo na bodi ya matangazo kubwa kutokana na uwezo wakon ni sababu ipi hata hivi leo kiwanja chetu hakina bodi ya matangazo kujua ndege gani inakuja na ndege gani inaondoka na hali yakuwa tunasema tunahudumia kimataifa.

Mhe. Waziri wa Miundo Mbinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba huduma za zimamoto zilizopo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Aman Karume hazipo chini ya mamlaka ya viwanja vile. Ni zimamoto ambayo inatoka kwenye Kikosi cha Zimamoto miongoni mwa Idara maalum za Serikali. Lakini huu ulikuwa ni utaratubu wa serikali.

Tunachofanya sasa hivi ni kuifanya Idara ya Anga kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Sheria hiyo ikishapitishwa hapa na kuidhinishwa na Mhe. Rais basi huduma za Zimamoto za Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar na cha Pemba zitakuwa chini ya Mamlaka hiyo.

Ni kwa nini matangazo hayatoki kwenye vipaza sauti. Na vile vile ni kwa nini hakuna *light display board* katika viwanja vyetu vya kimataifa. Hii naomba nijibu kwa pamoja.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba matangazo yanayotolewa katika viwanja vyetu vyote viwili kile cha Pemba na hiki cha kimataifa cha Zanzibar hakuna matangazo yanayotoka kwenye vipaza sauti. Lakini hii imetokana na ukosefu wa *system* zenyewe pale kiwanjani. Lakini ukosefu huo haukizuii kiwanja hichi kuwa cha kimataifa.

Kama nilivyotangulia kusema kwamba haya ambayo yanatakiwa yawepo pale inakuwa ni ngumu sana kama ni Idara ya Serikali. Idara ya Anga inayoshughulikiwa viwanja vya ndege ni idara ya serikali. Waheshimiwa mtakumbuka kwamba hali ilivyo katika Idara za Serikali ni tofauti na mamlaka inayojitegemea hata kama ni ya serikali.

Mwezi wa nne mwaka huu kuna mtaalamu atakuja kutuwekea *system* maalum na namuhakikishia Mheshimiwa mwakilishi kwamba pale kutakuwa na *system*

hiyo ya vipaza sauti popote ambapo mtu yupo, kutatolewa matangazo na yatakuwa *automatic.* Tutakuwa na *display board* ya *fly* zote nje na ndani. Pale ambapo watu wanatizamwa mizigo yao na. usafiri wao na ndani katika *lounge departure*.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ni kwamba *terminal three is under constructions* ni jengo jipya la abiria ambalo sasa hivi linajengwa kwa mkopo kutoka *Exin Bank* ya China na linakadiriwa kumalizika baada ya miezi 18. Tutakuwa na taminal tatu, hii ni ya zamani ambayo ipo sasa hivi na hii iwe ya tatu. Baada ya kukamilika ujenzi huu basi kiwanja chetu cha ndege kitakuwa na *system* nzuri zaidi hata kuliko ya Dar-es-Salaam. Kwa maana ya kuwa na Zimamoto ya *category* 8. sasa hivi tuko *category* (7) lakini wakati huo itafikiwa kiwango cha *category* 8 kutokana na vifaa ambavyo vinaletwa.

Lakini si hayo tu, matangazo na mengine yote ambayo yanakamilisha uzuri na hesma kubwa ya jina hili basi yatakuwa yamekamilika. Namuomba Mhe. Mwakilishi akubaliane na miye kwamba tumerithi vitu ambavyo sasa hivi ni lazima tufanyie marekebisho. Ni urithi huo ambao sasa hivi tunao lakini tunaurekebisha ili kuhakikisha kwamba tunakwenda na wakati.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Ismail Jusa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, sifa ya kuwa na kiwanja cha Ndege cha Kimataifa ni pamoja na kuhakikisha kunakuwa na taratibu nzuri na kanuni zinafuatwa ambazo pamoja na mambo mengine zinahakikisha usalama lakini pia nidhamu katika viwanja vyetu.

Mhe. Spika, swali langu ni kwamba kumekuwa na matumizi mara nyengine yasiyoeleweka ya chumba cha wageni mashuhuri (VIP) katika Uwanja wa Ndege wa Kimaifa wa Abeid Amani Karume. Tunawaona watu ambao kitaratibu unaelewa kwamba hawastahiki kutumia sehemu zile lakini imekuwa ni kawaida kwa hapa Zanzibar mara nyengine utawaona wafanyabiashara wakubwa, mara nyengine marafiki wa watu tu.

Sijui Wizara imejipanga vipi kuona katika kipindi hiki cha kuimarisha viwanja vyetu vya Ndege na kuwa kweli Kiwanja cha Kimataifa kinachosimamia kanuni zake, kinakomesha utaratibu huu na kwamba wale tu wanaostahiki kwa mujibu wa kanuni na sheria ndio wanaotumia sehemu hizi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Miundo Mbinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, VIP ambazo tuzitumie pale zipo mbili. Kuna VIP ambayo wanaondokea safari viongozi wakuu. Naamini amekusudia Chumba maalum chenye hadhi ya VIP kinachotumika kwa safari watu ambao si hao.

Ni kweli kuna mazoea kwamba chumba kile kinatumika si vizuri na sivyo inavyotakiwa. Hii ni kutokana na muhali, uzoefu, kujuana kwa viongozi wengi hata kama wamemaliza muda wao. Pale kuna *instruction* na ni toleo kabisa. Kwanza linasema suala la kupekuliwa hili naomba niliongeze katika kujibu swali hili.

Mhe. Spika, viongozi ambao hawatakiwi wapekuliwe ni viongozi watano, wamejatwa kabisa nao ni Mhe. Rais, Makamo wa Kwanza, Makamo wa Pili, Spika, na Jaji Mkuu. Wengine wote wanatakiwa wapekuliwe. Kwa hivyo ni vizuri waheshimiwa mawaziri, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge wafahamu kwamba hiyo ni sheria ya pale.

Mimi sioni sababu kwa nini uwe mkali, utake watu wafukuzwe kazi, watu wahamishwe kwa sababu umepekuliwa. Kama uko safi ni kwa nini ukatae kupekuliwa. Kwa hivyo wasi wasi kwa wale ambao wanakuwa wakali, wanapitisha watu wasiookuwa na hadhi ya kupita pale kwa kuwachukua kwenye ndege moja kwa moja kupita nao VIP, kuna mushkeli mkubwa.

Ningeomba sana viongozi wenye tabia hiyo. Kwa sababu kuanzia juzi utaratibu huo unaendelea, wasijewakaona wanaambiwa Mheshimiwa tukupekuwa au huyu hastahiki kama alivyosema Mheshimiwa juzi. Wafanyabiashara wote, wazoefu ambao tumewazoea pale wala sio viongozi wa serikali lakini kwa sababu tu ni wafanyabiashara ambao wamezoeleka huko nyuma, tunawaandikia rasmi kwamba kuanzia sasa wao hawatastahiki kama ambavyokuwa walikuwa hawastahiki kutumia VIP.

Waheshimiwa wote wawakilishi, wabunge, mawaziri, tunaorodha kutoka Idara ya Mamambo ya Nnje. Orodha hiyo ambayo tutaitumia katika kukubali mgeni au mtu au kiongozi kutumia VIP ambayo imekusudiwa kuelezwa hapa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kabisa kwamba viongozi wote tuliokuwepo hapa na ambao hawapa hapa, wajue kwamba kama hatukufuata sheria basi nchi hii itakuwa na sheria lakini zitakuwa hazifuatwi. Tukubali kwamba kila mtu ana wakati wake. Kama wako umemalizika hutakiwi tena uwepo pale basi tafadhali usiendi pale kwa sababu watu watafanya kazi kwa mujibu wa sheria tena kwa uratibu mzuri tena, sasa wasijewakaonekana wabaya.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe nadhani tutakubali maswali haya yamechukua muda mrefu sana na tunaweza tukashindwa katika muda uliopangwa.

Nam. 63

Vituo vya Kulipia Umeme

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Utaratibu unaotumika wa kulipia umeme kwa maeneo yote ye Unguja na Pemba ni wananchi kulipia huduma hiyo katika Afisi kuu za Shirika, jambo ambalo linawapa usumbufu wananchi wanaokaa maeneo ya mbali.

(a) Je, Kwa nini Shirika la Umeme lisianzishe utaratibu wa kufungua vituo vya kulipia umeme katika Wilaya ili kuwapunguzia wananchi gharama za usafiri na usumbufu mwengine wanaoupata.

(b) Kwa kuwa mara nyingi malipo ya umeme yanapofanywa katika Afisi kuu ya Gulioni, Unguja huwa na msururu wa foleni, Je, Wizara haioni kuwa huo ni usumbufu kwa walipaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuna usumbufu wa wananchi kugharimika kwa usafiri kufuata huduma ya malipo Afisi Kuu, hata hivyo Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme tayari wameshaanza mikakati ya kuhakikisha vituo vya kulipia umeme vinakuwepo maeneo tafauti. Hivi karibuni kinategemewa kufunguliwa kituo cha kununulia umeme wa Tukuza huko Mkokotoni na hatua zinachukuliwa kuanzisha vituo vyengine maeneo ya Bububu, Kiembesamaki, Gamba, Mahonda, Makunduchi kwa Unguja na kwa Pemba ni maeneo ya Mtambile na Konde.

(b) Mhe. Spika, mara nyingi msururu wa foleni ya malipo hutokezea pale Shirika linapotowa indhari ya kukata umeme kwa wenye madeni maeneo fulani. Tunawashauri wananchi wawe na kawaida ya kulipia bili zao na mapema ili kuepuka usumbufu huo. Aidha, wananchi wa maeneo ya mashamba, Shirika la Umeme linaendelea kuwafuata

wateja wake kwa njia ya magari na kupatiwa huduma hiyo ya malipo huko huko walipo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize swali la nyongeza Naibu Waziri.

Kwa kuwa wananchi wengi wa maeneo ya vijijini wanahitaji huduma hii ya umeme. Tatizo kubwa linalowasumbua ni umasikini yaani wanashindwa kuweza kupata pesa za pamoja za kugharimia ule uungaji wa umeme kuingiza ndani.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao kwa kuwakopesha huduma ile ya kuungisha umeme ndani ili walipe kidogo kidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli wananchi wengi wanashindwa kujisogezea huduma hii ya umeme. Lakini Shirika la Umeme limetoa mikopo kwa wananchi wote ambao wanataka kuunganishiwa umeme. Lakini nathubutu kusema labda tu wananchi hawa hawajafika katika shirika hilo.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii. Juu ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza.

(a) Kwa nini hadi hivi leo Shirika lako linatumia mifumo miwili ya malipo kwa wateja wake ule mfumo wa kukadiria na ule mfumo wa kileo.

(b) Je, huoni kwamba kutumia mifumo hiyo miwili ule mmoja wa kukadiria ndiko kunakosababisha manung' uniko na usumbufu kwa wananchi au wateja wako.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, si kweli kama Shirika linatoa bili kwa wananchi kwa makisio. Isipokuwa wananchi wengi hujisahau pale wanapotumia umeme na kutumia vifaa vikubwa ambavyo vinasababisha kutumia umeme mwingi na pale tu wanapopelekewa bili zao wanajisahau kama wametumia umeme mwingi na wakaona kama Shirika linawadhulumu. Lakini pale wanapofika ofisini hufanyiwa hesabu na wakapewa usahihi wa matumizi yao.

Kwa hivyo shirika letu naamini bado linakwenda katika mfumo mzuro na wala hakuna tatizo lolote wala dhuluma inayofanyika kwa mwananchi.

Mhe. Makame Mshimba Mbrouk: Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri. Katika jibu lake alililojibu alisema kuwa ni kweli shirika linatoa mikopo kwa wale waliokuwa tayari wanaotaka kutia umeme.

Je, atakubaliana na mimi kuwa mikopo hiyo inatoka kwa watu kujuana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Si kweli kama mikopo hiyo inatolewa kwa ujuano, hili nakataa. Kwa sababu shirika limetoa mikopo hiyo katika awamu zilizopita kwa vijiji takriban vyote kwa kila mteja ambaye alikuwa anafika pale Shirikani alikuwa anapatiwa huduma hiyo ya mkopo.

Nam. 86

Eneo la Tunguu Kusogezewa Miundo Mbinu.

Mhe. Fatma Mbarouk Said - Aliuliza:-

Serikali kwa nia safi imepima na kugawa viwanja katika eneo laTunguu kwa ajili ya makaazi ya wananchi, Ujenzi wa Vyuo Vikuu na Afisi za Serikali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Miundombinu ya bara bara, umeme na maji ili kuufanya mji huo kukuwa haraka na kuweka sura mpya ya Zanzibar ya leo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kawaida wizara ilipaswa kabla kugawa viwanja hivyo miundo mbinu hiyo iwe imeshafikishwa. Napenda kumtaarifu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu kupitia Shirika la Umeme tayari imeshaanza kuchukua hatua ya kusambaza huduma ya umeme na maji eneo la Tunguu na baadhi ya wananchi wameanza kutumia huduma hiyo. Wizara yangu itajenga mradi mkubwa wa maji kwa msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) katika eneo hilo pamoja na maeneo ya jirani. Lengo la wizara yangu ni kuhakikisha kuwa eneo lote lililopimwa viwanja hapo Tunguu linapatiwa huduma zote muhimu.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar Dr. Ali Moh'd Shein katika kampeni zake za kuomba ridhaa kwa wananchi aliahidi kwamba barabara ya Mwanakwerekwe Fuoni hadi Tunguu ataipanua.

Je, Mhe. Waziri unalijua hilo na kama unalijua ni lini barabara hiyo itajengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, labda tu niseme suala la barabara sio la Wizara yangu.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Waziri, Je, ni sifa zipi zinazotumika na wizara yako katika kugawa viwanja vya serikali kwa wananchi. Kama sifa hizo zipo ni wafanyakazi wangapi wa serikali ambao tayari wameshapata viwanja hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kuhusu viwanja hatutoi kwa wafanyakazi wa serikali. Isipokuwa viwanja vinastahiki kutolewa kwa mwananchi yeyote ambaye ameomba kiwanja hicho kupitia wizara yetu.

Nam. 9

Utekelezaji wa Mradi wa Maji Safi na Salama wa Akra

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Mradi wa maji safi na Salama wa AKRA ambao umelenga kusaidia wananchi wa majimbo matatu ya Mfenesini, Kitope na Bumbwini pamoja na kufikia hatua nzuri, kuna taarifa kuwa kwa hivi sasa umekwama.

(a) Je, ni tatizo gani lilokwamisha kukamilika kwa mradi huo.

(b) Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Mkanyageni, kupata huduma ya maji safi na salama.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mradi wa AKRA Maji na Usafi wa Mazingira unasaidia Majimbo ya Mfenesini, Bumbwini, Kitope na Donge bado utekelezaji

wake haujakwama ila *speed* yake imepungua kwa sababu baadhi ya vifaa havijafika nchini, mara tu vifaa hivi vikifika kazi yake itaendelea na maeneo yale yaliyokusudiwa kusambaza maji safi na salama yatahudumiwa.

(c) Kuhusu usambazaji wa maji Mkanyageni mradi huu hauhusiani na Mkanyageni au na eneo la Mkanyageni. Lakini kama kuna tatizo kwamba Mkanyageni hakuna maji wizara yangu italishughulikia tatizo hilo kadiri ya uwezo utakapopatikana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo.

(a) Mradi wa AKRA ni mradi uliokusudiwa kusaidia majimbo matatu na sasa hivi tayari visima vitatu vimechimbwa Mfenesini na vimeshatiwa pampu na mabomba yameshasambazwa. Lakini tunasikia kwamba fedha za kukata barabara ambayo visima vipo Selem kwa hivyo barabara ya Mkokotoni ikatwe ili iene kwenye tangi lililojengwa Michungwa miwili, fedha hizo hazijalipwa ndio mradi umekwama.

(b) Wananchi wa Mkanyageni mradi wa AKRA umepita kwenye jimbo langu kuanzia Shehia ya Mwakaje, shehia ya Mfenesini, Chuini, Mbuzini, Kama na Shehia ya Kihinani imepata mradi kutoka Japani, lakini kipande cha Mkanyageni kutoka Mkanyageni kwenda Mndo wawe hawakupata miradi yote miwili. Je, hawa watasaidiwa vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika,

(a) Si kweli kwamba Serikali haina fedha za kulipa ukataji wa barabara ili mradi uendelee. Tatizo liliopo baadhi ya vifaa havijafika na vipo njiani vitakavyofika mradi utaendelea.

(b) Kuhusu ombi la Mkanyageni kama eneo halikuingizwa katika mradi na kila mradi, hasa mradi wenye fedha za kigeni unafanywa *feasibility study*, unafanywa *quantity survey*, unafanyiwa utafiti kamili na makisio. Kwa hivyo huwezi kuchukua pesa za mradi wa hapa ukazipeleka huku. Tunachokifanya ni kutekeleza yale yaliyokisiwa.

Nilipokuwa najibu suala la (a) nimesema kama Mkanyageni mradi huo haujafika serikali yenyewe italishughulikia suala hili kwa kadiri ya uwezo wake utakapotengemaa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi katika kijiji cha Kitope ndani kuelekea Mbaleni kuwa mpaka sasa hivi mabomba hayajafika.

a) Je, hakubaliani na suala hilo kuwa mradi umelala.

b) Na hivi sasa barabara ya Mfenesini imeshakatwa na mabomba yameshalazwa. Je, Mhe. Spika, atakubaliana na mimi suala hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, suala la mradi kukata barabara imeshatekelezwa lakini bado mradi umelala. Mimi nasema sikubaliani nae kutokana na majibu niliyokwishakujibu wakati namjibu Mhe. Ali Abdalla Ali kwamba kinachosababisha mradi uchelewe kidogo ni kutokana na vifaa kwamba bado viko njiani havijafika. Mhe. Spika, naomba Mheshimiwa akumbuke kwamba siku hizi kuna matatizo ya baharini ya unyanganyaji wa mali wanaofanya Wasomali.

Mhe. Spika, njia za kusafirishia vitu sasa imekuwa ni ndefu kukimbia kasoro hizo, na ndio iliyosababisha vifaa hivi vichelewe kufika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi awe mstahamilivu madhali mradi huu upo tutahakikisha kwamba yale maeneo yaliyotajwa ndani ya mradi yatakamilika kwa hali na mali wakati vifaa vitakapofika nchini.

Mhe. Spika, pia nakubaliana nae kwamba Kitope mabomba yameshalazwa na wakati ukifika maji nayo yatafika kwa wananchi wa Mbaleni Kitope na kadhalika.

Nam.73

Ujenzi wa Vituo vya Afya

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inawahimiza wananchi kujenga vituo vya Afya katika kila Shehia, na kwa kuwa wananchi wa Shehia ya Ukutini, Jimbo la Chambani wameitikia wito wa Serikali kwa kujenga kituo cha Afya cha kisasa tokea mwaka jana.

(a) Je, kuna sababu zipi zinazokwamisha juhudi za Serikali kupeleka vifaa na madaktari wa kutosha kwenye kituo hicho hali inayopelekea usumbufu kwa wananchi wa sehemu hiyo.

(b) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa kitendo cha wanachi kufuata matibabu katika hospitali ya Abdalla Mzee na Chake-Chake kunapelekea usumbufu usio wa lazima kwa wananchi wa Shehia ya Ukutini ambao wangeweza kupata huduma ya awali ya matibabu Kijijini.

(c) Je, Wizara inatoa ahadi gani ya kuliondosha tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu :-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.73 lenye (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza ningependa nimjulishe Mheshimiwa kuwa Sera ya Wizara ya Afya haitilii sana mkazo wa kuongeza idadi ya vituo nchini bali lengo liwe ni kuimarisha huduma katika vituo vilivyopo hili nimelisema tangu juzi.

Naomba Waheshimiwa mtusaidie kuelekeza nguvu zetu kuboresha vituo viliopo, na tuongeze vituo pale tu mazingira yanyapolazimisha kufanya hivyo. Mfano mzuri ni Shehia ya Cheju ambapo kipo kituo cha afya, lakini nyumba ya daktari haikumalizika kujengwa. Kituo cha Ukutini kiko Wilaya ya Mkoani na kule kunatakiwa kuwe na vituo vya afya 15, na katika vituo vilivyoko huko vituo 4 ambacho ni Kengeja, Bogoa, Wambaa na Ukutini hivyo ni vituo vya *PHCU+* vile nilivyovizungumza juzi ambavyo vinatakiwa viwe na wafanyakazi wake, kuwa na huduma ambazo ni 10 na wafanyakazi 7. Kwa hiyo unachokiomba hapa ni kidogo zaidi kuliko tulichokipanga.

a) Sababu zinazokwamisha kupeleka wafanyakazi ndio zile zile nilizozizungumza juzi, nafikiri tulielewana kwa hiyo ufinyu wa bajeti ambao wafanyakazi na maslahi duni ndio matatizo tuliyonayo

b) Ni kweli kuwa huduma za awali zinapaswa kutolewa katika Kituo cha Ukutini ili kuwaepusha kufuatia huduma hizo Chake na Mkoani. Jitihada zitafanywa kuhakikisha kuwa tatizo hili linamalizika.

c) Kwa muda huu tumewapangia madaktari wa vituo vya Chambani na Mtangani kwenda kutoa huduma kwa wiki mara mbili. Kwa hiyo huduma inapatikana pale kwa siku 4 wale wanakwenda mara nyingi kutoka Chambani na kutoka Mtangani wanakwenda mara mbili.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi nataka Mheshimiwa akumbuke kwamba kituo hiki cha Ukutini kipo kati kati baina ya Shehia ya Ngwachani, Shehia ya Chambani, Shehia ya Mtangani pamoja na Shehia ya Kiwani. Kwa hivyo, kutokana na umuhimu wa kituo hiki kuzungukwa na shehia hizi na kwa sababu jana katika maelezo yako ulisema kwamba kuna wahitimu wengi wa Chuo cha Afya karibu asilimia 70 wanatoka Pemba. Ni mipango gani Mheshimiwa uliopanga katika wizara yako ili kuwapeleka hawa Wapemba waliomaliza mafunzo hapa kule Pemba kufanya kazi.

Mhe. Spika, nikizungumza hivi naomba nitoe maelezo kidogo Wizara ya Elimu kwa kiasi fulani imetusaidia kuna walimu wengi wa Pemba wameomba nafasi kusomesha hapa Unguja sasa hivi wamepunguza lile zogo la upungufu wa walimu pale Pemba. Kwa hivyo, kutokana na hali hii wizara yako imejipanga vipi kutusaidia Wapemba katika vituo hivi muhimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza nasema hivi kuwa tusibaguane Wapemba na Waunguja hakuna sababu tulishatoka huko tunaendelea mbele sote ni Wazanzibari na vituo vya afya vya Zanzibar vyote vinahitaji wafanyakazi.

Kuhusu suala la kwamba Shehia zinakuzunguka nilichokisema ni kuwa kituo cha Ukutini kitakuwa na huduma bora nyingi za kuweza kuhudumia hizo shehia zote zilizokuzunguka. Kwa hivyo, usiwe na hofu wafanyakazi 7 na huduma 10 ni nyingi kwa sababu hicho ni kituo cha *PHCU+* sio tu kituo cha kawaida kina na nyongeza ya huduma. Naomba sasa nikutajie hizo huduma ili uzielewe.

Mhe. Spika, tumesema zitakuwa ni huduma za msingi za wagonjwa wanawake na uzazi.

- Huduma za dharura za wagonjwa wanawake na uzazi.
- Kutayarisha rufaa ya mgonjwa kwenda hospitali ya Wilaya pale ambapo tatizo liko nje ya uwezo wa kitaalamu.
- Huduma kwa mtoto aliyezaliwa.
- Huduma kwa mzazi kabla ya kujifungua.
- Huduma baada ya ujauzito kuharibika.
- Huduma za vijijini kuhusu afya ya mama na wajawazito.
- Huduma za maabara.
- Huduma za meno.
- Huduma za ushauri nasaha kwa hiari.
- Huduma za afya ya akili kwa mtu mmoja au kikundi.
- Elimu ya afya ya akili.

- Utambuzi wa matibabu ya msingi ya maradhi ya akili.

Mhe. Spika, anataka nini tena Mhe. Mwakilishi. Wafanyakazi utakaokuwa nao katika kituo chao ni:

- Daktari Msaidizi.
- Muuguzi Msaidizi.
- *PHND* wawili.
- Muhudumu wa Afya ya kinywa cha afya na meno mmoja.
- Muhudumu wa usafi mmoja.
- Bwana afya au bibi afya atakayepatikana mmoja.
- Fundi sanifu wa madawa.

Sasa tuzungumze kuhusu wafanyakazi, ni kwamba sikusema kama asilimia 75 wamehitimu, nimesema wanafunzi walioko chuoni hivi sasa ni asilimia 75 wanatoka Pemba. Lakini pia nilisema kuna baadhi ya wanafunzi wameshahitimu hivi sasa ambapo kuna maombi yao nusu wanatoka Unguja na nusu wanatoka Pemba.

Nimesema hivi kwamba wale ambao watakaotoka Pemba tutahakikisha wanakwenda huko na wale wanaotoka Unguja kwa uhaba ulivyo kule Pemba wa wafanyakazi nao watakwenda miaka miwili. Kwa hivyo, wale wote ikiwezekana na ikiwa nyinyi hamtoturudia kinyume mkasema huyu nirudishieni Unguja basi watakwenda huko Pemba kwa sababu mkataba wa Wizara ya Afya unasema ntafanya kazi popote.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa miongoni mwa vijiji vilivyohamasika kujenga vituo vya afya ni pamoja na kijiji cha Kibokoni kilichoko katika Jimbo la Wawi. Na kwa kuwa jiwe la msingi la kituo hiki liliwekwa na aliyekuwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Dk. Ali Moh'd Shein) ambaye sasa ni Rais wetu mpenzi wa Zanzibar. Kwa kuwa ujenzi wa kituo hiki tayari umemalizika bado mambo ya *plastering, ceiling, painting* pamoja na kupeleka vifaa na madaktari.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini wizara yako itamalizia ujenzi wa kituo hiki.
b) Kwa kuwa kituo hiki ujenzi wake umamalizika zamani na tayari jengo hili linaendelea kuchakaa. Je, kuendelea kuliacha vile si matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi.

Mhe. Spika: Utaratibu wa kuchupia maswali kidogo unaleta matatizo, maana tutapata maswali ya Makangale, tutapata maswali Kangani huku, tutapata

maswali ya Nungwi ilimradi tu hatwendi pale kwenye swali mama, hebu tafuta utaratibu wa kuuliza swali mama juu ya kijiji chako na hiyo *dispensary* unayojenga.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi amejibu kama kuna wahitimu wengi wa afya ambao wakimaliza kusoma watapelekwa kule Pemba ili waende wakafanye kazi huko. Mhe. Spika, ni kwamba kuna mtindo wa madaktari kuchukuliwa wakipelekwa Pemba wanakataa kufanya kazi kwa sababu hawataki kukaa kule Pemba.

Je, Mhe. Naibu Waziri kwa sababu umesema mkataba wenu wa kazi unamuonesha mfanyakazi wa afya kufanya kazi mahala popote anapopangiwa ni lini hasa suala hili la madaktari kupangiwa sehemu wende wakakae kule Pemba wakakataa watalikomesha.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, wanafunzi wa Wizara ya Afya wanakwenda kuomba wenyewe kwa hiari Chuo cha Afya na wanachangia kusomeshwa, wanapomaliza wengine wanakuja Wizara ya Afya kuomba kazi, wengine wanakwenda private na mtu yuko huru kwenda anakotaka. Kwa hivyo, yule atakayekuja Wizara ya Afya serikalini tunamwambia kwamba ajira yetu iko huku, nguvu zetu kwa sasa tunataka tuzipeleke Pemba kwa sababu kule kuna uhaba wa madaktari.

Kwa hivyo, kama kaja mwenyewe serikalini hana sababu ya kuchagua kwa sababu mkataba uko pale, hivyo tunakupangia nafasi ya kukaa. Mhe. Spika, mimi sioni sababu kwa nini mtu kwenda kwao kufanya kazi, jamani mtu kwao. Sasa kama hataki ina maana hapo ndio hataki kazi atakwenda kutafuta kazi nyengine, siwezi kumlazimisha kwamba lazima nikupeleke huko lakini hiari na mkataba ndivyo unavyosema.

Nam. 67

Wafanyabiashara wa Zanzibar Kutozwa Kodi Tanzania Bara

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa wafanya biashara wa Zanzibar wamekua wakilalamika kutozwa kodi mara mbili wanapopeleka bidhaa zao Tanzania Bara, baada ya kulipa kodi hiyo Zanzibar.

(a) Mhe. Waziri, ni sababu zipi zinazopelekea wafanyabiashara hao kutozwa kodi mara ya pili wanapofika Tanzania Bara.

(b) Je, kuna hatua zipi zilizochukuliwa na Serikali kuondosha tatizo hilo na zimefikia wapi kiutekelezaji huku wafanyabiashara wetu wakiendelea kulalamika kuwepo kwa tatizo hilo.

(c) Je, Kwa nini wafanyabiashara kutoka Tanzania Bara wao wanapoleta bidhaa zao hapa Zanzibar hawatozwi kodi kwa mara mbili.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, **Viwanda na Masoko -** Alijibu:-

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 lenye vifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili katika bandari ya Dar-es-Salaam. Mhe. Spika sababu kubwa ya kutozwa kodi katika bandari hiyo ni kuwa baadhi ya watendaji wa *TRA* Dar-es-Salaam walikuwa wanadai kwamba bidhaa zinapoingia Zanzibar kutoka nje huwa hazitozwi kodi sahihi kulingana na kiwango kinachotakiwa kulipwa. Hivyo bidhaa hizo zinazopelekwa Dar-es-Salaam hulazimika kulipwa tena.

b) Mhe. Spika, zipo hatua kadhaa zimechukuliwa katika kulifuatilia suala hili zikiwemo kufanyika mazungumzo baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia vikao vya Makamo wa Rais na vikao vya Baraza la Biashara la Zanzibar. Hatua hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kutatua matatizo hayo.

c) Mhe. Spika, ni kweli wafanyabiashara wanapoleta mizigo yao kutoka Tanzania bara huwa hawalipi kodi kwa mujibu wa Sheria isipokuwa wanalipa ada za bandari. Aidha, wafanyabiashara kutoka Zanzibar nao pia wanatakiwa kulipa ada kama hizo za bandari katika bandari ya Dar-es-Salaam**.**

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni kwamba kwa sasa wakati umefika wakuweza kukaa pamoja kwa mara nyengine tena kuweza kukiondosha kile kitengo ambacho kimewekwa pale Dar es Salaam, kitengo ambacho hakipo kwa mujibu wa sheria kwa sababu hata nyaraka ambayo inatumika katika kupatia malipo hiyo mizigo ambayo inatokea

Zanzibar nahisi sio nyaraka halali kwa matumizi ambayo yanafanyika pale Dar es Salaam. Kwa sababu nyaraka ambazo wanatumia tunaita katika mtandao wa *custom* kwamba ni *transfer form*. Kazi kubwa ya transfer form ni kuweka takwimu katika masuala ya mizigo inayohaulishwa kutoka sehemu moja kwenda nyengine.

Lakini wao Bara kwa kutumia nyaraka hii hii wanatumia kuwatoza kodi Wazanzibari ambao wanaondosha mzigo sehemu moja kupeleka sehemu nyengine ya Muungano.

Je, Mhe. Waziri mmejipanga vipi katika hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, **Viwanda na Masoko:** Mhe. Spika, ni kwamba sisi Wizara ya Biashara ndio kwanza tunaipata taarifa hiyo tungemuomba basi aje tukae nae ili tuweze kulifuatilia hili na kulifanyia kazi.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara sio wa kweli na baadhi ya wafanyakazi wa *TRA* sio waaminifu. Je, Mhe. Waziri umeliona suala hilo na kulijua na kama ndio wizara yako ina mkakati gani ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, **Viwanda na Masoko:** Mhe. Spika, ni kweli kumekuwa na matatizo ambayo ameyasema Mheshimiwa ya kutokuwa waaminifu kwa wafanyakazi na kutokuwa wa kweli kwa wafanyabiashara. Mhe. Spika, wafanyakazi wa *TRA* ni kwamba wizara imejiandaa kulifanyia kazi suala hilo kwa kukaa vikao na Afisi za *TRA* kuzungumzia suala hili kuhusu baadhi ya wafanyakazi wao ambao sio waaminifu. Lakini pia wizara yetu tumekuwa tukikaa mara kwa mara na wafanyabiashara ili kuzungumzia matatizo yanatokea kutokana na shughuli za biashara za kila siku.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kuwa kuna *minimum* ya Zanzibar na kuna *maximum* ya Bara, *minimum* ya Zanzibar haifanyikazi Bara lakini *maximum* ya Bara inafanyakazi hapa. Je, suala hilo Mhe. Naibu Waziri wizara yako itaweza vipi kulifuatilia ili wananchi wa Zanzibar wanapokwenda kule wasiweze kulipa mara mbili.

Mhe. Waziri wa Biashara, **Viwanda na Masoko:** Mhe. Spika, suala la kulipa mara mbili katika Bandari ya Dar es Salaam juzi Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Raisi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ameeleza kwa urefu sana hapa kwamba kwa mujibu wa sheria bandari ya mwanzo ndio inayostahiki kulipa

kodi. Kwa hivyo, mzigo unaokuja Zanzibar ina maana umeshalipiwa kodi na haustahiki kulipiwa kodi tena mara mbili. Hizi ni moja katika kero zilizokuwepo na mazungumzo katika kero za muungano na kupitia ngazi ya juu hizi tayari zimeshatatuliwa.

Mpaka *TRA* wamepelekewa barua rasmi kuwapelekea wafanyakazi wao wote. Kuna baadhi ya wafanyakazi wa *TRA* walioko Tanzania Bara ni kwamba hawataki kutimiza yale yaliyozungumzwa katika vikao hivyo ya kuondoa kero za Muungano. Tena tunawaambia wafanyabiashara kwamba wasilipe kodi tena mara mbili, tunawaambia unapolipa kodi tuletee hizo risiti na *document* za kulipwa kodi, lakini bado wafanyabiashara hawajatuletea. Kwa hivyo, ili kukabiliana na suala hili tunataka mashirikiano ya dhati baina ya wafanyabiashara wa Zanzibar na wizara yangu ili tupate document kwani hatuwezi kuzungumza kwa mdogo tunataka tuzungumze kwa vielelezo.

Mhe. Spika, tunaamini mpaka jana wako wafanyabiashara ambao wanasema kuwa wamelipa bidhaa mara mbili, wamelipia Zanzibar na wamelipia Dar es Salaam. Mhe. Spika, ikiwa hivyo ni kweli basi itakuwa hapa pana unafiki baina ya sehemu mbili hizi. Kwa hivyo, sisi tunataka tuondoe huo hivyo tunataka mashirikiano ya wafanyabiashara wetu.

Nam. 76

Upandishaji Bei za Bidhaa Muhimu

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2010 kumalizika na Mheshimiwa Rais kutangaza Baraza la Mawaziri, Wazanzibari walisikia na kushuhudia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ikikataa na kupiga marufuku uingizaji wa vyakula visivyo na kiwango kwa matumizi ya binaadamu kama vile Mchele, Unga, Mafuta n.k. Hatua hii ya Serikali ilipongezwa sana na wananchi, lakini punde imekuwa ni kilio baada ya bei ya vyakula kupanda mfano: Mchele uliouzwa TShs. 800 – 900/= sasa unauzwa TShs. 1,000 – 1,200/= kwa kilo huku wafanyabiashara wakidai kuwa hayo ni matokeo ya Serikali kupiga marufuku vyakula visivyo na kiwango.

(a) Nini kauli ya Serikali kutokana na kadhia hiyo.

(b) Vyama vyote viwili vilivyounda Serikali ya Umoja wa Kitaifa vilijigamba kwamba vitaleta vyakula vya bei nafuu na vyenye viwango pindi vikiingia madarakani. Kwa kuwa ndoto ya kuingia

madarakani imetimia, ni lini wananchi watatumia matunda ya kura zao kwa kununua vyakula vyenye bei nafuu na viwango.

(c) Kwa nini Serikali haiweki utaratibu wa kutangaza bei za bidhaa muhimu kama Mchele, Unga wa Ngano, Sukari, Mafuta n.k. katika Soko la dunia angalau wiki mara moja, ili kuwaelimisha wananchi na kuzuia ujanja wa wafanyabiashara wanaopandisha bei za bidhaa kiholela.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 lenye vifungu (a) (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa mara baada ya Uchaguzi Wizara ya Biashara, Viwanda, na Masoko imekataza na inaendelea mpaka sasa kukataza na inapiga marufuku uingizaji wa bidhaa hasa vyakula visivyokuwa na viwango vinavyokubalika kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

(a) Mhe. Spika, suala la kuongeza bei vyakula mara baada ya Uchaguzi Mkuu kulisababishwa na mambo mawili makubwa. Kupungua kwa uagiziaji bidhaa ndani ya kipindi cha Uchaguzi Mkuu na pia ilitokana na kupanda kwa bei za bidhaa hizo katika soko la dunia. Serikali ilichukua hatua kwa kuzungumza na wafanyabiashara juu ya kuongeza uagiziaji wa bidhaa na kuwashauri kupunguza bei ya bidhaa hizo kwa wananchi. Juhudi za kuongeza idadi ya wafanyabiashara watakaoleta vyakula nchini kutoka nje ya nchi na Tanzania Bara zinaendelea na hivyo itasaidia sana kupunguza mfumko wa bei ya vyakula nchini.

(b) Mhe. Spika, sote hapa tumekuwa ni mashahidi wiki iliyopita baada ya kuupitisha kwa kauli moja Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chombo cha Kusimamia Viwango vya Bidhaa. Mhe. Spika, chombo hicho kitakuwa na mamlaka ya kuweka viwango vya bidhaa zote zinazozalishwa na zinazoingizwa nchini, ambapo wafanyabiashara na wananchi kwa juumla watatakiwa kutumia viwango hivyo vya bidhaa vilivyowekwa.

(c) Mhe. Spika, katika suala la kutangaza bei tayari wizara imeandaa utaratibu wa kutangaza bei za bidhaa zikiwemo bidhaa muhimu kama vile mchele, unga wa sembe, unga wa ngano, sukari, mafuta pamoja na bei za bidhaa nyengine zinazozalishwa hapa nchini vikiwemo viazi, mihogo, ndizi na matunda. Matangazo hayo

yamekuwa yakisikika kila siku kuanzia tarehe 21 mwezi wa Januari saa 11 kamili za jioni. Matangazo hayo Mhe. Spika, yatakuwa yanatolewa vile vile katika vipindi vya televisheni na vijarida maalum vitakavyokuwa vinatolewa na Wizara ya Biashara.

(d) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa, suala la umimi (*monopoly*) katika biashara ni moja kati ya mambo kadhaa yanayosababisha matatizo ya uhaba wa vyakula, bei kubwa ya bidhaa, kuwepo kwa vyakula visivyokidhi kiwango vinavyokubalika kisheria. Lakini Mhe. Spika, kama nilivyosema awali, wizara iko katika mchakato wa kuifanyia mapitio sheria ya kumlinda mlaji Nam.2 ya mwaka 1989, ili kuleta ushindani halali katika biashara. Ni matumaini ya serikali kuwa, utekelezaji na usimamizi mzuri wa sheria hiyo utaondosha matatizo yanayosababishwa na umimi katika biashara.

Mhe: Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana na baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuwa amesema wizara sasa hivi inajitahidi kuzungumza na wafanyabiashara ili kuleta bidhaa haraka iwezekanavyo. Anaweza akawaambia Wazanzibari kuanzia bidhaa ambazo zitaingia karibuni bei za vyakula zitakuwaje? Mchele wanakusudia kuuza shilingi ngapi na sukari badala ya shilingi elfu mbili ya hivi sasa.

(b) Tuna taarifa kwamba wafanyabiashara ambao wamepewa kibali cha kuingiza bidhaa za vyakula wamebaguliwa, yaani wametengwa wale ambao wana uwezo zaidi. Je, kwa sasa Zanzibar kuna wafanyabiashara wangapi ambao wizara yake imetoa vibali kwa ajili ya bidhaa hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, namuomba arudie swali lake la (b) sijalisikia vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Swali (b) Mhe. Spika, nilitaka kujua tu kwa sasa Zanzibar tuna wafanyabiashara wangapi ambao wamepewa kibali cha kuingiza bidhaa za vyakula kama mchele, unga na mafuta.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, si rahisi sasa hivi kusema bei ya vyakula ambavyo hata bado hapa nchini havijaingia kusema itakuwa kiasi gani. Ningemuomba Mhe. Mwakilishi tukasubiri vyakula

hivyo kwanza viiingie nchini, vikishafika tutakaa pamoja na wafanyabiashara na kuangalia jinsi gani bidhaa hizo za vyakula bei zake zitakavyokuwa.

Lakini jibu (b) Mhe. Spika, pia sikulisikia vizuri.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa vile hakulisikia vizuri jibu la pili naomba nimsaidie Naibu Waziri wangu. Ameuliza kwamba masuala ya wale watu kupewa vibali vya kuleta bidhaa nchini. Wizara ya Biashara kwa mujibu wa sheria haihusiki na kutoa vibali vya uletaji wa vyakula nchini. Kwa mujibu wa sheria ya chakula, madawa na vipodozi ni bodi ndio inayoshughulika na kutoa vibali vya wafanyabiashara kuleta vyakula nchini.

Hata hivyo, inaonesha kwamba bodi hii bado haijafanya usajili wa wale watu ambao wanaleta bidhaa hizo nchini. Inavyoonesha kwamba hakuna utaratibu huo mpaka sasa uliofanywa na wale wote ambao wanaleta vyakula hawajapewa vibali, kila mfanyabiashara alikuwa huru kuleta bidhaa yake hapa na hakuna aliyezuiwa. Kilichojitokeza ni kwamba, baadhi ya wafanyabiashara kama wanane mpaka kumi ndio waliojijengea ustaarabu au *monopoly* ya kuleta bidhaa nchini au ukiritimba. Lakini sisi Wizara ya Biashara tunasema kwamba hakuna mpaka hivi sasa mipaka au uchaguzi, kila mfanyabiashara mwenye uwezo aidha mdogo, mkubwa au wa kati tunasema alete bidhaa nchini bila ya vikwazo vyovyote, ilimradi afuate sheria inavyosema.

Sheria iko wazi kwamba kila mtu anayetaka kuleta bidhaa za vyakula, madawa na vipodozi aende Wizara ya Afya katika Bodi ya Madawa akafanye usajili tu basi, naamini kwamba kila mtu atatumia fursa hiyo ili alete vyakula bila ya ubaguzi wowote. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umekwisha na maswali matatu yamebaki na kesho ni siku ya mwisho. Nilikuwa namuangalia Mhe. Waziri hapa naona bado hajafika, tuitumie nafasi hii tuyamalize maswali haya kwa kutoa hoja kuwa tuyamalize wakati waziri anajitayarisha haraka sana kuja ili tuendelee na mswada wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliotengwa kwa mujibu wa kanuni hautoshi kumaliza maswali yaliyoko kwenye *order paper* ya leo, naomba kutoa hoja kuweka kando muda wa maswali ili tuweze kumalizia maswali yaliyomo katika *order paper* ya leo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono. Wanaokataa hoja, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri jana nilifurahi kuonakwamba bidhaa mbovu zinatoswa baharini ili kuepusha athari kwa walaji. Je, Mhe. Naibu Waziri bidhaa zile hazitoathiri viumbe wa baharini.

Swali langu jengine ni kwamba je, wafanyabiashara ambao wanatuletea bidhaa mbovu ni adhabu gani watapewa ili kukomeshwa kutuletea bidhaa mbovu kila siku hapa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli jana tumeona sote katika vyombo vya habari bidhaa ambazo hazikukidhi haja ya viwango zimeshaharibika vikiangamizwa baharini.

Mhe. Spika, katika hatua iliyochukuliwa pale vyombo vyote vinavyohusika vinakuwepo na kwa hivyo, kiusalama inaonekana kwamba hakuna matatizo kwa kuvitosa vyakula vile ambavyo vinaonekana kuharibika ndani ya bahari. Kwa hivyo, hakuna madhara ambayo yatatokea kwa kuvitosa vyakula vile baharini. Kwa sababu sio kwamba vina madawa lakini vilikuwa vimefikia *expire date*, vimekuwa vimeshaharibika.

Swali la pili Mhe. Spika, adhabi zipo kwa watu wanaoleta bidhaa ambazo zimeshapitwa na wakati na adhabu hizo huwa zinachukuliwa kufuatana na taratibu zilizowekwa na vyombo vinavyohusika.

Nam. 66

Serikali kusaidia Walimu wa Qur-Ani

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Walimu wa vyuo vya *Qur-an* wana mchango mkubwa sana katika kuinua elimu na maadili ya jamii. Hata hivyo, kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu yanayosababishwa na kutopata msaada wa kifedha kutoka serikalini.

(a) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba, umefika wakati sasa serikali ikawaangalia walimu hawa kwa jicho la kuwasaidia huku ikifahamu mchango wao katika jamii.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia angalau posho kwa mwezi ili waweze kujikimu kimaisha.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilsihi swali lake Nam. 66 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Vyuo vya *Qur-an* vina mchango mkubwa sana katika kuinua elimu na maadili ya jamii. Pia ni kweli kuwa walimu wa vyuo hivyo wanafanya kazi kubwa na muhimu katika maendeleo ya jamii. Aidha, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa walimu wa vyuo hivyo wanaishi katika mazingira magumu na wanastahiki kupatiwa misaada mbali mbali.

Wizara yangu imekuwa ikivipatia misaada mbali mbali Vyuo vya *Qur-an* licha ya kuwa vyuo hivyo vina milikiwa ama na mtu binafsi, jamii au jumuiya. Misaada ambavyo tumekuwa tukivipatia ni mafunzo ya mbinu za ufundishaji kwa walimu wake na misaada ya misahafu na mabusati. Hata hivyo, naomba ifahamike kuwa Vyuo vya *Qur-ani* vitaendelea kuendeshwa na watu binafsi, jamii au jumuiya. Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Ni kweli kwamba serikali ina wajibu wa kuwasaidia walimu wa vyuo vya Qur-ani, ndio maana kipo kitengo maalum pale afisini kwangu yaani wizarani.

b) Wizara yangu haina mpango wa kuwalipa posho la kila mwezi walimu wa vyuo vya *Qur-ani*. Jukumu hilo ni la wazazi wanaopeleka watoto wao katika vyuo hivyo kama wengi wetu tuliopo hapa tulivyosoma kwa kulipia mafingu baada ya kuhitimu.

Napenda kutoa wito kwa wananchi, wafanya biashara kuendelea kuwasaidia walimu wa vyuo vya *Qur-ani* ili waweze kuendelea kuwafunza watoto wetu katika hali ya utulivu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika kutoa maelezo yake alisema anapata misaada mpaka ile ya kutoa mafunzo kwa walimu wa vyuo vya *qur-ani.* Je, Mhe. Waziri ni walimu wangapi katika Jimbo la Mkwajuni uliwahi kuwapatia mafunzo haya.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kitengo kinachoshughulikia vyuo vya *Qur-ani* kutoka katika wizara yangu, huwa kinawakusanya walimu hao kwa kufanya semina. Sasa kwa jumla siwezi kumjibu kwamba ni wangapi, kwa sababu katika maeneo mengi wameshapita na wameshatoa mafunzo hayo kuwasaidia kuwapa mbinu.

Nam. 38

Zanzibar Kupata Uanachama wa *FIFA*

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo katika Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Waziri wa Habari aliyemaliza muda Mhe. Ali Juma Shamuhuna ilifanya kazi nzuri ya kuipigania Zanzibar kupata uanachama wa *FIFA*.

Je, wizara yako ina mikakati gani ya kuendeleza juhudi hizo ili Zanzibar iweze kupata uanachama huo wa *FIFA*.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo katika Serikali ya Awamu ya Saba iliendeleza juhudi zilizofikiwa na wizara iliyokuwepo chini ya serikali ya awamu ya sita, katika kufuatia juhudi zilizokwisha kuchukuliwa za kuhakikisha kwamba Zanzikbar inapata uanachama wa *FIFA*.

Mhe. Spika, juhudi zilizochukuliwa na wizara hii katika awamu iliyopita ni kubwa na kwamba kazi iliyobakia hivi sasa ni kusubiri uamuzi wa *FIFA* au kuhimiza kupatiwa uamuzi huo pale itakapobidi kufanya hivyo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kupigania kupata nafasi kuwa mwanachama wa *FIFA* ni suala ambalo lina faida kwa nchi mwanachama husika. Kwa sababu ukiwa mwanachama wa *FIFA* unapata faida ya kushirikia katika mashindano mbali mbali ambayo yanaandaliwa na *FIFA*, halikadhalika kupata ruzuku ya kila mwaka zaidi ya dola laki mbili na nusu kwa kuweza kuendeleza miradi mbali mbali, kujenga viwanja pamoja na mafunzo ya ualimu na waamuzi na mambo mengine.

Sasa Mhe. Spika, Zanzibar ndio tupo katika mbio ya kupigania nafasi hiyo kwa kuleta maendeleo ya mpira wa miguu Zanzibar. Lakini kwa kupitia mgongo wa *TFF*, Zanzibar imeweza kufaidika na faida hizo za *FIFA* kwa kuweza kusaidiwa kujenga uwanja wa bandia kule Kisiwani Pemba katika uwanja wa Gombani. Naishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kutoa Dola laki moja na elfu ishirini katika kuchangia mradi huo wa kujenga uwanja wa nyasi za bandia pale Kisiwani Pemba katika uwanja wa Gombani.

Je, namuuliza Mhe. Naibu Waziri, mradi ule umefikia wapi na utamalizika lini. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: *Shukran.* Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Mjumbe arudie swali lake.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, namuuliza waziri kwamba Zanzibar tumepata msaada wa *FIFA* katika zile faida za *FIFA* kupitia mgongo wa *TFF*, kwa kupata msaada wa kujengewa uwanja na kutiwa nyasi za bandia Kisiwani Pemba katika uwanja wa gombani. Je, mradi ule ambao serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu ya sita iliweza kuchangia dola laki moja na elfu ishirini katika kujenga uwanja huo wa Gombani. Je, mradi ule umefikia wapi na utamalizika lini ili timu zetu ziweze kutumia uwanja ule.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tulipata msaada huo na juhudi hizo bado zinaendelea, ingawaje zimekwama kidogo tu kutokana na usagaji wa kokote zile, mashine imeharibika. Lakini tumo katika mbio za kuimaliza ile mashine ili iweze kufanya kazi vizurina tuendelee na mradi. Natumai labda miezi miwili ijayo basi shughuli zitakuwa tayari zimeshamalizika.

Nam. 80

Utunzaji wa Lugha na Lahaja

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Wataalamu wa lugha Barani Afrika wanatueleza kuwa Bara hili lina lugha na lahaja zinazotambulika zaidi ya 22,000. Lakini kutokana na utandawazi na maingiliano ya jamii lugha na lahaja hizo zinapotea siku hadi siku na kupoteza uasili wake katika jamii na makabila mbali mbali.

(a) Je, Mhe. Waziri, Zanzibar tunazo lugha na lahaja ngapi za asili.

(b) Ni kwa kiwango gani lugha na lahaja zetu zimeathirika kutokana na utandawazi na maingiliano ya jamii.

(c) Ili kulinda lugha na lahaja zetu ni lazima tuwe na nyenzo na kwa upande wetu Kamusi ni miongoni mwa nyenzo muhimu zitakazosaidia kuzilinda lugha na lahaja zetu. Kama hivyo ndivyo, ni lini Wazanzibari watakuwa na Kamusi zao za lahaja za Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Zanzibar tuna lugha moja ya Kiswahili na lahaja tatu ambazo ni Kitumbatu, Kimakunduchi na Kipemba.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kuwa Kiswahili na lahaja zake zimeathirina na utandawazi na maingiliano ya jamii.

- Mhe. Spika, athari kwa upande wa Kiswahili zinaonekana katika maana na matumizi ya maneno. Maendeleo ya kiteknolojia na utandawazi yamesababisha baadhi ya maneno kutojulikana, kutotumika au kutumika vibaya. Maneno kama vile hando, chano, kinoo, kiwe hayatumiki sana.
- Neno kama mida na mapungufu yanatumika vibaya. Aidha, maingiliano makubwa ya kijamii yamesababisha watu kuacha kutumia maneno ya asili yanayojulikana na badala yake kutumia maneno mengine, mfano: Mkaa badala ya makaa, shule badala ya skuli, majitaka badala ya maji machafu, hela badala ya pesa na kadhalika.
- Athari pia inaonekana katika kiwango cha matamshi na miundo ya sentensi. Mfano wa miundo hiyo ni kama yote kwa yote, mwisho wa siku, achukue nafasi yake, dakika tano kabla ya saa saba na mengineyo.

Mhe. Spika, kutokana na utafiti mdogo na wa haraka haraka tulioufanya, viwango vya athari hizo ndani ya lahaja vinatafautiana.

- Kwa upande wa lahaja ya Kimakunduchi asilimia 40 ya lahaja hiyo imeathirika.
- Lahaja ya Kipemba athari yake inakisiwa kuwa asilimia 30.

- Athari katika lahaja ya Kitumbatu sio kubwa sana ikilinganishwa na Kimakunduchi na Kipemba. Inakaisiwa kama asilimia 15. Hii inatokana na kutokuwepo kwa maingiliano makubwa ya watu wanaotoka na kuingia ndani ya Kisiwa cha Tumbatu.

(c) Mhe. Spika, kwa sasa hatuwezi kusema hasa ni lini tunaweza kuwa na makamusi hayo, lakini juhudi kubwa zimechukuliwa kufikia lengo hilo. Tayari tuna rasimu ya miswada ya makamusi ya lahaja zote tatu ambayo iko tayari kwa kuchapishwa wakati wowote zikipatikana fedha. Tumejaribu kuomba Ufadhili wa *UNESCO,* lakini bado hatujapata jibu la kutia moyo. Fedha zinazohitajika kuchapisha alau nakala elfu mbili kwa kila lahaja ni milioni thamanini na saba (87,000,000/=).

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika,baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali la nyongeza. Mhe. Spika, yuko mwimbaji wa Kimasai aliyeimba nyimbo ya *Bongo Flavor* na akasema mimi ni Mmasai na yeye anajivunia Umasai wake, na mimi Mtumbatu najivunia Utumbatu wangu na kwa hivyo napongeza kwamba kumbe Kitumbatu hakiathiriki sana.

Kutokana na kwamba Kitumbatu hakiathiriki sana, atakuwa tayari Mhe. Waziri kutuchukua sisi Watumbatu labda kutushawishi tukaowe Makunduchi na Pemba tukazidi kulinda hizi lugha zetu za lahaja.

Lakini swali la pili, Baraza la Kiswahili limedhibiti vipi mmong'onyoko wa lahaja zetu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, bado sijamsikia vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Baraza la Kiswahili hapa Zanzibar limedhibiti vipi mmong'onyoko wa lahaja zetu. Naomba kujibiwa hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli lahaja zetu za Kizanzibari yaani Pemba na Unguja ni lahaja moja wapo zilizokuwa sisi wenyewe wananchi huwa tunazipotosha. Sasa niwaombe Waheshimiwa wawe tayari kuelimisha jamii kuhusu lahaja zetu kwa mikoa yetu yote.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika jibu lake mama Mhe. Waziri amekubali kwamba Kiswahili kinaathirika kutokana na wakati wa sasa. Je Mhe. Waziri,

wizara yako ina mikakati gani kukilinda na kukiendeleza Kiswahili chetu ili kisipotee kabisa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, wizara yangu ina mipango mikakati ya kuweza kuendeleza Kiswahili cha Zanzibar ili kisipotee.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo naomba kuongezea jibu.

Ni kwamba Baraza la Kiswahili kwanza ukifanya Kiswahili kisipotee kimetoa kamusi rasmi ya Kiswahili fasaha Zanzibar na ipo madukani na inapatikana. Wametayarisha kitabu cha Utamaduni wa Mswahili, nacho pia kipo na kinapatikana. Kitu muhimu ni kuzoea sisi kujifunza na kusoma vitu hivi ili Kiswahili tukijue kwa usahihi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Nimpongeze Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kauli yake ya kukuza Kiswahili chetu. Mhe. Spika, Kiswahili ni lugha ambayo pia inatumika katika mitihani yetu zaidi ya mawasiliano. Uchunguzi ninaofanya ni kwamba, pamoja na kuwa sisi Wazanzibari tunaambiwa ndio asili kabisa wa lugha hii ya Kiswahili, lakini tukiangalia matokeo ya mitihani tunayofanya wenzetu wa Bara tunaona hivi sasa wanatushinda kwa matokeo.

Je, ni kwa sababu wao hawakijui hiki Kiswahili chetu kuwa sisi ndio shina, au kuna mabadiliko ambayo sisi tumeshindwa kukabiliana nayo katika kukuza hii lugha yetu mpaka matokeo yakawa si mazuri sana kiasi hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, sikusikia hata kidogo swali lake kwa kweli.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nilivyosema ni kwamba, inavyosemekana Zanzibar ni chimbuko la lugha ya Kiswahili na katika mitihani yetu tunayofanya mmo ni wa Lugha ya Kiswahili, lakini tukiangalia matokeo ya wanafunzi wetu hasa kwa kiwango hiki cha *'O' Level.* Wenzetu wa Bara takriban kwa wastani wanapasi zaidi kuliko sisi, swali ni kwamba.

Je, ni kwa sababu sisi hatukikuzi hiki Kiswahili kimazingira mpaka tukaweza kufanya vizuri kama wao, au kuna sababu zipi nyengine ikawa kwenye shina matokeo si mazuri zaidi kuliko kule ambako hakuna shina la lugha hii.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naomba kwa idhini yako kusaidia jibu la swali la Mhe. Salim Abdulla Hamad kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, pamoja na kuwa Kiswahili ni lugha yako lakini unataka kufanya mtihani lazima usome. Kama unategemea kwamba wewe umezaliwa nacho tu Kiswahili bila ya kusoma ukaona wale wamahiri wa Kiswahili namna walivyotunga vitabu na walivyokitumia Kiswahili kwa kupanga zile lafudhi na mambo mengineyo bila shaka mtihani utakushinda.

Mhe. Spika, wenzetu walioko Tanzania Bara wanafahamu kwamba wana matatizo katika lugha ya Kiswahili kwa hivyo wanafunzi wao wanasoma sana kuliko tunavyotumia sisi nafasi hii kusoma.

Mhe. Spika, pili ni kwamba tunayo jitihada sasa hivi ya kuhakikisha kwamba Kiswahili sanifu ndio kinatawala Tanzania. Hii ni changamoto ambayo bila shaka itakuwa inaleta matatizo kidogo kwa wengine ambao wenye shahada za Kiswahili kufikia makubaliano watumie Kiswahili kipi, kile kinachotumika Zanzibar, au kinachotumika Tanzania Bara, au kinachotumika Kenya. Mhe. Spika, tatizo hili lipo lakini Mabaraza haya yanakaa kitako na ninahakikia siku moja yatafikia makubaliano na watakubaliana hasa lahaja zitumike zipi.

Mhe. Spika, kusema kweli Kiswahili cha Zanzibar hizo siku za nyuma cha mjini Unguja ndicho kilichoamuliwa kwamba Kiswahili fasaha. Lakini sasa hivi kila mtu anasema ana Kiswahili fasaha. Lakini *inshaallah* watu wetu watafika pahala na watakubaliana na ndio maana Baraza la Kiswahili wakatunga hili kamusi la Kiswahili ambao nao walipata tabu kulifanya mpaka likachapishwa na likaingia katika maduka. Hivi sasa wanaendelea kufanya kazi hiyo na nawapongeza sana. Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo azifikishe pongezi kwa Baraza la Kiswahili kule kwamba wanafanya kazi nzuri sana na nategemea wataweza kuleta mafanikio sana. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi angalau nielezee kidogo kuhusu mswada wetu huu wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, kabla sijenda kwenye sheria yenyewe naomba niliarifu Baraza lako tukufu kwamba ni vyema tukaelewa katika mjadala huu tunazungumzia utumishi wa umma. Hii tusichanganyishe na ile Sheria ya Kazi *(Labour Law)* ambayo ni sheria iliyopitishwa katika Baraza lako tukufu Sheria Nam. 11 ya mwaka 2005 inayoitwa *Employment Act.*

Mhe. Spika, sheria hizi mbili ni tofauti ingawa zina maudhui yaliyokaribiana sana. Sasa unapoisoma *Employment Act* Nam. 11 ya mwaka 2005 inazungumzia utaratibu wa uajiri wenyewe pamoja na haki zile za uajiri. Pia inazungumzia suala la *machinery* ya uwekaji wa mshahara pamoja na *disciplinary measures* ambazo zinaweza zikachukuliwa katika hiyo. Hii ni tofauti kidogo na Sheria ya Utumishi ambayo inazungumzia masuala ya maadili ya utumishi, usimamizi wa utumishi na kuanzishwa kwa Kamisheni ya Utumishi pamoja na mambo ambayo yanahusiana na hayo.

Sasa haya yote Mhe. Spika, usimamizi wa utumishi pamoja na usimamizi wa wafanyakazi, masharti ya ajira ndio yanayolenga mswada huu ambao tunauzungumzia.

Mhe. Spika, kulikuwa na mawazo au baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walizungumzia kwamba kuna matatizo kidogo katika mswada huu na katiba kwamba zinagongana. Mhe. Spika, naomba nielezee tu kwamba katiba inatoa miongozo ya jumla katika masuala mazima, lakini katiba hiyo hiyo utaona katika vifungu vyengine inasema kwamba ni sheria ambayo itatumika katika kuendeleza miongozo ile ambayo imetolewa.

Mhe. Spika, ukichukua tafsiri hiyo inaonesha dhahiri kwamba katiba na sheria hii hakuna mgongano ambao unazungumzwa au kama ulivyokuwa ukizungumzwa. Kwa hiyo, sheria madhumuni yake ni kufafanua ile miongozo ambayo imetolewa ndani ya katiba.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie kidogo kuhusu sheria yenyewe ya utumishi. Mhe. Spika, katika sheria hii naomba kwanza tutazame kifungu cha 51 cha Katiba ya Zanzibar ambayo inatoa Madaraka ya Serikali kwa Rais. Naomba kunukuu inasema kwamba “Rais anaweza kukasimu madaraka hayo kwa mtu mwengine yeyote yule”.

Kwa hiyo, suala ambalo lilizungumzwa katika sheria hii la kuonesha kwamba kuna kukasimu baadhi ya mambo kwa Rais kwenda kwa Katibu Mkuu Kiongozi au kwenda kwa Waziri anayehusika, lile lilikuwa haligongani na katiba kama baadhi ya wajumbe walivyokuwa wana wasi wasi nalo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hii ni dhahiri kwamba katika masuala kama haya Mhe. Rais ana kazi nyingi na lazima kisheria apewe nafasi ya kuweza kukasimu madaraka ambayo yeye mwenyewe ataona mtu gani anahisi kazi zile anazotaka kuzifanya angeliweza kuzifanya. Kwa hiyo, kifungu hichi hakikumfunga Rais kwamba lazima akasimu madaraka kwa Waziri au kwa Makamo wa Rais au kwa fulani. Lakini yeye mwenyewe atakapoona kwamba huyu nitakayemkasimia madaraka anafaa kwa hiyo anao uwezo huo.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo ukitazama hii sheria pia na ukitazama katiba inasema kwamba Mtendaji Mkuu katika Shughuli za Utumishi wa Umma atakuwa ni Rais kwa mujibu wa katiba. Sasa kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba kuna *system* mbili, kuna *Parliamentary System* na *Presidential System*. Kwa wenzetu ambao wana *Parliamentary System* utaona Waziri Mkuu ndie Mtendaji Mkuu na kwa maana hiyo *Chief Secretary* wao anakuwa chini ya Waziri Mkuu.

Mhe. Spika, hii haina tofauti na kwamba sisi tunatumia *Presidential System* na Mtendaji Mkuu kwa Shughuli za Serikali ni Rais kwa hiyo msaidizi wake katika suala hili ni yule mtendaji ambaye yuko katika ofisi yake na hapa atakuwa ni Katibu Mkuu Kiongozi. Sawa sawa na *Parliamentary System* ambayo kuna Waziri Mkuu na *Chief Secretary* na huku ni Rais ambaye msaidizi wake kwa masuala ya Shughuli za Utumishi atakuwa ni Katibu Mkuu Kiongozi.

Kwa hiyo ukitazama hayo Mhe. Spika, ni kwamba Katibu Mkuu Kiongozi kwa mantiki hiyo, kwa utaratibu huo ni kwamba yeye atamsaidia Mhe. Rais katika masuala ya utumishi. Kwa sababu Rais ndie aliyepewa jukumu hilo la kwamba yeye ni Mkuu wa Utumishi katika Serikali.

Mhe. Spika, kulikuwa na maelezo kwamba pengine kifungu cha 11 cha mswada kinagongana na kifungu cha 43 (5) cha katiba. Mhe. Spika, kifungu cha 43 (5) cha katiba kinaonesha tu kwamba mtendaji yeyote ambaye amepewa jukumu kwa sababu hili ni suala la utumishi. Kwa hiyo, yeye atawajibika kufuata ngazi na hatimae kwenda kwa Rais kwa sababu yeye ndio Mtendaji Mkuu.

Lakini hii haina maana kusema kwamba Baraza la Wawakilishi kama walivyoonesha wengine kwamba ndilo linalofanya check and balances au linalosimamia serikali. Kwa sababu hapa kuna mambo mawili, kuna *individual responsibility* ambayo ni ya yule mtendaji anayefuata mdorongo ule wa moja kwa moja anaripoti mpaka kufikia kwa chombo cha juu.

Lakini kwa ujumla maelezo yote au mambo yote yale yanayofika hata kwa Rais, Rais yeye ni Kiongozi wa shughuli zile za Utumishi, ndio Kiongozi Mkuu. Madaraka yale ambayo yamepewa Baraza la Wawakilishi katika suala la *check and balance* yapo katika kifungu cha 43 (5) cha katiba kwamba hata kama utakwenda katika mkondo huo wa *individual responsibility*, basi mwisho *collective responsibility* ya wizara zote pamoja na serikali ile itawajibika katika Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo Mhe. Spika, kifungu cha 11 cha mswada hakina matatizo ya kugongana na kifungu cha 43 (5) cha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pia kulizungumziwa suala la utumishi kuwa na uhusiano wa utumishi wa kisiasa katika kifungu cha 6 cha mswada huu. Mhe. Spika, naomba nilitaarifu Baraza lako tukufu kwamba ukisoma kifungu cha 6 (2)(a) kinasema wazi kwamba sheria maalum itatungwa katika usimamizi wa kisiasa. Kwa hiyo, hii haina maana kwamba yameingiliana isipokuwa mswada huu unaelekeza kwamba kuwe na sheria ambayo inazungumzia masuala ya utumishi wa kisiasa.

Lengo la kuweka utaratibu huu Mhe. Spika, ni kwamba ni vizuri mwanasiasa anafanya kazi katika suala la shughuli za umma ingawa yeye katika upande wa kisiasa. Lakini sheria inaelekeza kwamba anapoingia katika shughuli zile basi kuwe kuna utaratibu maalum ambao yeye mwenyewe anaujua kwamba anatakiwa afanye hichi na hichi ili awe katika mstari wa kuendeleza shughuli zile. Ndio maana kifungu cha 6 (2)(a) kinaweka wazi kwamba kutakuwa na sheria inayohusiana na utumishi wa kisiasa kwa utaratibu huo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 14 kimeelezea majukumu ya Katibu Mkuu Kiongozi na kifungu cha 80 (2)(a) kinatoa wasi wasi wote kuwa mtumishi amezibwa mdomo. Kwa sababu hapa kulikuwa na maelezo kwa baadhi ya wajumbe kwamba kifungu cha 80 (2)(a) labda kimemziba mdomo au kimeziba midomo wale watu wanaohusiana na kazi. Kwa mfano, jumuiya zile za *OTTU* na kama hizo.

Sasa Mhe. Spika, ukikisoma kifungu 80 (2)(a) kinasema wazi wazi kwamba "Kutakuwa na kanuni ambazo zitatungwa kwa ajili ya kuweka utaratibu ambazo kanuni hizo zitahusu vyama vya wafanyakazi na shughuli zao na namna gani wanaweza wakapeleka matatizo yao katika serikali".

Kwa hiyo, kifungu hichi kimeweka wazi au kimetoa uhuru kwa vyama hivyo vinavyowatetea wafanyakazi kwamba wao wanaweza kutetea wafanyakazi wao kwa kupitia njia hizo.

Mhe. Spika, pia kulikuwa na mazungumzo yaliyokuwa yakizungumzwa kuhusiana na kifungu cha 36 (5) cha mswada ambacho walisema kwamba kinakiuka au kina dalili ya kukiuka kifungu cha 5 A (3) cha katiba.

Mhe. Spika, kifungu cha 5 A (3) cha katiba kinazungumzia suala la *Separation of Powers* yaani mihimili ile mitatu ambayo ni Serikali, Baraza la Kutunga Sheria pamoja na Mahakama. Wakasema kwamba mswada huu katika kifungu cha 36 (5) kinaonesha kama kinagongana na kifungu cha 5 A (3).

Mhe. Spika, vifungu hivyo vilisomwa kwa pamoja. Utaona wazi kwamba nafasi ambayo alipewa waziri anayehusika na utumishi wa umma ni nafasi ya kutafuta ushauri kwa hii mihimili mingine. Kwa hiyo, unapotafuta ushauri kwa mihimili mingine haina maana kwamba unaingilia kazi katika mihimili hiyo. Ni utaratibu wa kawaida kwamba mtu yeyote ambaye anapewa dhamana anaweza akatafuta ushauri pahala popote ambapo anahisi panafaa. Sasa huu ni ushauri tu na haugongani na kifungu cha 5 A (3) kama ilivyoonekana.

Mhe. Spika, pia ukisoma kifungu cha 57 (8) ambacho kimeweka wazi utaratibu mzima wa wafanyakazi, namna wafanyakazi wale wanaweza wakapandishwa daraja au wakapewa mambo mengine ya onyo au ya kutoa maelezo yao. Hili lilizungumzwa sana katika mantiki ya *appraisal*.

Mhe. Spika, ninachopenda kusema ni kwamba kwa maana hiyo hasa ile maana aliyoizungumza Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba kifungu cha 57 (8) ukikisoma kinaonesha wazi kwamba *appraisal* hizo zinaweza zikafanywa kwa kutumia kifungu hichi ambacho kimewekwa.

Kwa hiyo Mhe. Spika, ninachotaka kusema ni kwamba mswada huu wa utumishi ni mswada ambao umeelezea zaidi na umeongezea nguvu ile sheria niliyoitaja mwanzo Nam. 11 ya mwaka 2005 ya *Employment Act.* Sasa tunapokuwa na sheria mbili hizi ya *Employment Act* na Sheria hii ya Utumishi wa Umma hapo unaufanya utumishi katika serikali kuwa na utaratibu mzuri ambao zamani ulikuwa haupo.

Kwa maana hiyo Mhe. Spika, mimi napenda niseme tu kwamba ni sheria ambayo imeanzisha kitu kizuri, najua kwamba matatizo yanaweza yakatokea katika kutekeleza sheria hii. Lakini hivyo ndivyo sheria zote zilivyo lazima matatizo yatajitokeza, pale ambapo yatajitokeza basi tunaweza tukayarekebisha hapo ambapo yanatokea.

Kwa maana hiyo Mhe. Spika, napenda na mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Mgogoni niunge mkono mswada huu na tuuombee kheri upite ili tuweze kuutekeleza, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* naomba nikushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuchangia mswada huu muhimu wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kuwa waheshimiwa wengi wamepata kuuchangia mswada huu na mengi yamesemwa na kwa sababu Mhe. Abubakar Khamis Bakary ameshachangia yale maeneo ambayo nilitaka kuchangia kwa hiyo naomba nichangie katika maeneo matatu yafuatayo.

Mhe. Spika, eneo la kwanza ambalo naomba nilichangie kwanza ni mjadala wa mswada katika kamati. Mhe. Spika, naomba kwanza niishukuru na niipongeze Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri na ngumu waliyoifanya katika kuuchambua mswada huu muhimu. Mhe. Spika, kamati yako ilitumia siku tano nadhani katika kuufanyia haki mswada huu.

Mhe. Spika, shukurani za kipekee ziende kwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa juhudi kubwa aliyoichukua ya kuhakikisha kwamba mswada huu unakuwa mzuri kwa sababu alipitia miswada yote miwili wa Kiingereza na Kiswahili na kuhakikisha kwamba lugha iliyotumika katika miswada yote miwili inaoana. Kwa sababu miswada yote miwili sasa hivi Mhe. Spika, kama tulivyokubaliana kwamba itakuwa ni sheria na yote itatiwa saini. Kwa hiyo, kwa niaba ya ofisi yangu napenda nimshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia mswada huu katika kamati umepata bahati kubwa sana ya kujadiliwa au ya kuhudhuriwa na Jopo la Wanasheria. Mswada huu ulikuwa na wanasheria 6 akiwemo Katibu wa Baraza Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim, Mshauri Mkuu wa Baraza Ndugu Yahya Khamis Hamad akiwemo Katibu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Ndugu Nasra Awadh Salmin na Mwanasheria wa Wizara kwa wakati huo Ndugu Kubingwa, pia na Mhe. Ismail Jussa Ladhu lakini Mwenyekiti wake alikuwa akimwita Mwanasheria wa Kamati. Jopo hili Mhe. Spika, liliongozwa na mwenyewe Mwanasheria Mkuu ambaye alikuwemo kwenye kamati hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, zaidi ya hao niliowataja pia katika kamati kulikuwa na mzee wetu Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi Serikalini Mhe. Othman Bakari ambaye alitusaidia sana uzoefu wake kwenye mambo ya utumishi na alitupa busara zake hasa kuhusu utumishi wa umma.

Kwa hiyo Mhe. Spika, nataka kusema kwamba mswada huu tuliujadili kifungu kwa kifungu na ndio maana ukachukua siku nyingi na vile vile kama nilivyosema tulijadili miswada yote miwili ya Kiswahili na wa Kiingereza.

Mhe. Spika, kutokana na mjadala huo ambao ulikwenda katika kamati ndio maana tumekuja na mswada mwengine ambao ilibidi tuuchapishe ulikuwa na marekebisho mawili makubwa. Rekebisho la kwanza lilikuwa ni rekebisho la lugha ambapo kulionekana kwamba baadhi ya vifungu vya Kiswahili na Kiingereza haviendi sambamba ikabidi tuvirekebishe.

Lakini pia kulikuwa na marekebisho ya nadharia kwa hiyo ikabidi tulifanye hilo ili tukubaliane na hiyo nadharia iliyokuwemo. Tukakubaliana na tukaona kwa sababu marekebisho ni mengi tukaamua kufanya *version* mpya ambayo tumeileta ili iwe rahisi kwa Waheshimiwa Wajumbe kuweza kuufuata mswada ambao umekuja kuliko kuja na marekebisho tu yaliyofanywa kwenye kamati na mswada ule. Kwa hivyo, hiyo ilisaidia sana wajumbe katika kuufahamu mswada huu ambao tunao hapa.
Lakini pia kama alivyosema Mhe. Waziri katika uwasilishaji wake kwamba mswada huu kabla ya kuletwa Barazani hapa ulifanyiwa semina mbili, semina ya wajumbe wa kamati na ile semina ya wawakilishi wote. Mhe. Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba mswada huu kwa sasa hakuna kifungu hata kimoja cha sheria hii kinachopingana na Katiba ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, eneo la pili ambalo napenda nilizungumzie ni kile kifungu cha 6 cha mswada huu ambacho kinazungumzia uhusiano na utumishi wa kisiasa. Mhe. Spika, baadhi ya wajumbe waliochangia katika mswada huu waliomba kifungu hichi kiondoshwe au kifutwe. Napenda niwaeleze kwamba hata katika kamati tulipokuwa tunakijadili kifungu hichi kimetuchukua muda na kamati nayo ilipendekeza kifungu hichi kiondolewe. *(Makofi)*

Lakini baada ya majadiliano na baada ya kujibiwa kwa hoja nyingi ikaonekana kwamba tukibadilishe tu na si kukiondosha na ndio hicho tukaja na marekebisho hayo ambayo tumekuja nayo.

Mhe. Spika, kifungu hichi ambacho kinazungumzia uhusiano tulikiangalia kwa upana zaidi tukasema kwamba hii mihimili mitatu kuna Utawala, Baraza la Wawakilishi na Mahakama ambayo inafanya kazi lakini bado ina uhusiano. Uhusiano uko wa aina nyingi, tukichukua mfano wa hivi vyombo vitatu tunasema kuna Rais, lakini tukasema kwenye masuala ya itifaki akiondoka Rais anakuja Makamo wa Pili wa Rais, wakiwa wote wawili hawapo hao basi katiba inasema aje Mhe. Spika akaimu hiyo nafasi, kama hayupo na yeye basi aje Jaji Mkuu kuchukua hiyo nafasi. Wewe utaona hawa watu wana uhusiano katika mambo ya kuendesha serikali (utawala).

Lakini pia tukasema kuna uhusiano mwengine unatokea katika vyombo hivi vitatu na hasa kama sasa hivi tunavyojadili sheria. Sheria kabla ya kuja Barazani inaanza katika utawala, inabidi ipitishwe Baraza la Mapinduzi baada

ya hapo ndio inakuja Baraza la Wawakilishi, lakini ikitoka hapa inakwenda Mahakamani.

Kwa hiyo, Baraza la Mapinduzi linapitia sheria, likishapitia inaletwa Baraza la Wawakilishi na Baraza la Wawakilishi nao wana haki ya kuipitia na kuona je, hii iliyopitishwa kule inaendana na maslahi ya umma au haiendi, kwa hivyo maana inarekebishwa. Lakini pia na mahakama nayo ina uwezo wa kuiangalia je, hii sheria iliyopitishwa Baraza la Wawakilishi iko sawa na ndio maana wakati mwengine inapotokea matatizo, inabidi mahakama iseme iangalie madhumuni ya kupitishwa hii sheria na Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, tukasema huo uhusiano upo. Sasa tukasema lazima uhusiano wa utumishi wa umma lazima nao utakuwa na uhusiano japo kidogo na utumishi wa kisiasa. Kwa hivyo, ule mswada wa mwanzo ulikuwa umeundwa na kamati imewekwa pale ili kuangaliza zaidi uhusiano huo. Lakini uhusiano huo tulikubaliana kwenye kamati kwamba na kifungu kipya tuliokuja nacho tulisema kwamba kuna uhusiano wa mambo mawili yafuatayo.

Kwanza kwenye kanuni za maadili. Mhe. Spika, hapa tulikuwa na maana kwamba kikao chako hiki nadhani baadae mwezi wa Aprili utakuja mswada ambao unazungumzia rushwa na kanuni za maadili. Hizi kanuni za maadili Mhe. Spika, zitawahusu viongozi wa kisiasa na zitawahusu viongozi wengine wa umma. Kwa hivyo, hapa ndio tukasema hawa wanahusiana, kwa sababu wote hawa maadili yatawagusa. Ndio tukasema huu ndio uhusiano wao, kwenye hili watahusiano. Pale mwanzo ndio maana tukasema kuwe na kamati ione juu ya haya mahusiano yanakwendaje na hizi sheria tukasema kwanza zipitishwe kwenye kamati izione, lakini bahati mbaya kwenye kamati ikakubaliwa kuwa hiyo kamati isiwepo. Kwa hivyo, tukasema hapa kuna mahusiano na ndio maana hiyo tukaibakisha.

Jengine Mhe. Spika, tukasema kuna mahusiano kwenye sera za malipo, kwa sababu tukasema waheshimiwa wanasiasa wawakilishi na wengineneo wanapata mishahara na maposho na watumishi wa umma wanapata mishahara na maposho. Kwa hivyo, hapo pia pana mahusiano. Lakini tukasema uhusiano huu inabidi lazima uangaliwa, kwa sababu sasa hivi tumeona kuna matatizo, watumishi wenti kwa sababu ya maslahi madogo na mambo mengine basi wanaamua kuja kwenye siasa sasa. Hapa tuna baadhi ya mifano mizuri, somo yangu Omar Yussuf , alikuwa mtendaji mzuri tu wa umma, lakini akasema aah! Nadhani maslahi kule mazuri zaidi. Hata Dk. Mwinyihaji Makame na yeye yupo. Kwa hivyo, masuala kama haya ndio tukaona ni tatizo.

Pia kuna tatizo jengine Mhe. Spika, kama baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walivyosema, kwamba kuna wengine sasa wanaamua kwenda kwenye Bunge

zaidi kuliko Baraza la Wawakilishi, kwa sababu ya mafao na maslahi. Ndio tukasema hili ni suala ambalo hawa watu wanahusiana. Ndio tukasema haya mambo ni lazima uhusiano huu uwekwe sawa na uangaliwe katika utumishi wa umma na utumishi wa kisiasa.

Mhe. Spika, kutokana na hili ningewaomba wajumbe waione hiyo hali ya kifungu hiki na niwaombe kwamba bado tunadhani kifungu hiki kibaki kama kilivyo, kutokana na huu uhusiano ambao nimeueleza.

Mhe. Spika, labda suala jengine la tatu ninalotaka kulizungumzia hapa ni hili suala la Katibu Mkuu Kiongozi. Mhe. Spika, kamati yako ilichukua muda katika kujadili suala hili, na ilichukua muda kwa sababu mswada huu baadae tulibaini kuwa ulipotayarishwa, ilikuwa hakuna Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa hivyo, msimamizi wa utumishi alikuwa ni Katibu Mkuu Kiongozi. Kwa hivyo, baadae tukagundua kuwa sasa kuwe na wizara ambayo itahusika na utumishi wa umma na utawala bora, *roll* yake ni nini katika mswada huu. Tukagundua kwamba kweli Katibu Mkuu wa Utumishi na Utawala Bora pamoja na waziri madaraka yao yalikuwa hayako wizuri. Ndio maana ikabidi kuna vifungu vile ambavyo tunavirekebisha, tukasema hapana, madaraka haya sasa kwa sababu wizara ipo, lazima apewe waziri au Katibu Mkuu wake.

Mhe. Spika, kwa hivyo, hivyo vifungu ndio utaona kwamba katika mswada wa mwanzo, yale madaraka ambayo alipewa Katibu Mkuu Kiongozi, tukaona haya ni lazima yaondolewe na yawekwe kwenye wizara. Hicho ndio tulichofanya. Kwa vile vifungu ambavyo tunadhani mpaka sasa hivi yapo yale madaraka ambayo tumebakisha ya Katibu Mkuu Kiongozi, tukadhani kwamba kutokana na umuhimu wake na kutokana na majukumu yake aliyopewa kikatiba kwamba yeye ndio kiongozi wa utumishi wa umma, tukadhani kwamba yale madaraka bado yabaki kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, labda niseme tu kwamba katika kuangalia suala hili, kamati pia iliangalia uzoefu wa wenzetu nchi nyengine. Kama Mhe. Abubakar Bakar na Mhe. Ismail Jussa walivyosema, tuliangalia *system* ambazo wenzetu wanazitumia *Parliamentary* na zile *Presidential*, lakini tukagundua sisi tumechanganya hizi. Kwa hivyo, kutokana na mchanganyiko huo, ikabidi na sisi lazima tu-*balance* juu ya madaraka hayo ambayo yako kwa Katibu Mkuu.

Pia kuna Waheshimiwa Wajumbe wengine walikuwa wanatia mashaka kuhusu malipo ya Katibu Mkuu Kiongozi katika wakati wake wa kustaafu. Mhe. Spika, nadhani Mhe. Juma Duni Haji alisema kwamba watu tunaangalia sura. Mfano nyumba ya Spika inajengwa kule, lakini watu wanamuangalia Mhe. Kificho, sio Spika, lakini hawajui kama ni ya Spika.

Mhe. Spika, nadhani hapa tuone kwamba Katibu Mkuu Kiongozi, pia ni Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, ambaye anafanyakazi kubwa kwa ajili ya Baraza la Mapinduzi. Yeye ndiye mwenye kuhifadhi siri za Baraza na za serikali, lakini kama katiba inavyosema kuwa yeye ndiye kiongozi wa utumishi wa umma. Pia yeye ndiye mwenye kusimamia maslahi ya viongozi hawa wa Baraza la Mapinduzi.

Sasa Mhe. Spika, mtu wa namna hiyo wakati anapostaafu, wakati anajua wale anaowasimamia pale wanafuata nini. Kwa hivyo, na yeye kumuacha hivi hivi itakuwa hatumfanyii haki, hatufanyi haki kwa sababu kama nilivyosema ana majukumu mawili, yeye kama Katibu Mkuu Kiongozi, lakini pia kama Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningewaomba wajumbe wako nao walione hilo jukumu alilokuwa nalo la Katibu Mkuu Kiongozi kuwa kama ni Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, tuone kuwa hiyo stahili iliyowekwa hapo kwamba anastahili kupewa.

Mhe. Spika, kwa sababu mengi yamesemwa, naomba tu kwa kumalizia niseme machache. Moja niseme kwamba naomba nikubaliane na maelezo ya Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Makame Mshimba, kwamba yale maneno maslahi ya umma, nadhani yanahitaji kuwekewa tafsiri.

Mhe. Spika, kuna kesi ya polisi fulani walishtakiwa kule Tanzania Bara na wakaachishwa kazi kwa maslahi ya umma. Lakini walipokwenda mahakamani, mahakama ya kwanza ikayakubali, lakini walipokwenda mahakama ya rufaa ikatengua iliyoyahukumu, kwa sababu walisema neno maslahi ya umma halikutafsiriwa. Kwa hivyo, linawezekana likatumika vibaya. Kwa hivyo, na mimi nashawishika kwamba labda na hili tuliwekee tafsiri kwenye kanuni.

Mhe. Spika, jengine ambalo nadhani lilizungumzwa na Mhe. Hija Hassan ambalo Waheshimiwa Wajumbe wengi walililalamikia, ni hili suala la miswada kutokutimiza siku 21. Nadhani hili zaidi linahusiana na afisi yangu. Lakini labda niseme Mhe. Spika, kwamba huko mbele serikali tumejipanga kuwa tatizo hili tuliondowe, kwa sababu tunajua umuhimu wa Waheshimiwa Wajumbe kupata miswada katika siku 21 na zaidi, ni kuweza kupata maoni mengi ya wananchi wao.

Lakini Mhe. Spika, niseme tu kwamba suala la miswada ni kama zile mbio za *relay*, kwamba hiki sio chombo kimoja, kwa sababu tunajua kwamba mswada unaanzia kwenye wizara husika, halafu unakwenda kwenye kamati ya makatibu wakuu ambao mswada huu ukipita tutakuwa tumeshauhalalisha kisheria, halafu unapelekwa kwenye Baraza la Mapinduzi, baadae upelekwe kwenye Afisi ya Mwanasheria Mkuu uchapishwe na halafu ndio uletwe hapa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, mzunguko unakuwa ni mkubwa kidogo. Hivyo,

tunajaribu sasa ili kuona tunajipanga vipi, nadhani huko mbele tumejipanga vizuri, kwa sababu sasa hivi tutakuwa na orodha ya miswada ambayo inakwenda katika *cabinet*, kwa hivyo tutakuwa tunaijua mapema ili kuweza kutoa taarifa mapema.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema ni kwamba nadhani huko mbele tumejipanga kuwa tutajitahidi kuwa hizo siku 21 tuweze kuzifikia kwenye miswada ijayo mbele.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache, basi na mimi naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waupitishe mswada huu, ili uweze kuanza kazi na tuone matunda yake huko mbele. Mhe. Spika, ahsante sana *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kufanya majumuisho ya michango ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuhusu Mswada wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kujadili mswada huu na hadi kufikia muda huu ambao tunafanya majumuisho tukiwa na afya njema.

Pili naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kutuongoza vyema katika shughuli zetu hapa Barazani na hasa ulivyotoa fursa kwa kila mjumbe kuchangia kwa kadiri alivyoona inafaa. Lengo ni kuhakikisha kuwa tunapitisha sheria iliyo bora kwa utumishi wa umma na kwa maslahi ya nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waliochangia kwa kusema na kwa maandishi, kwa michango yao mizuri katika kuufanya mswada huu uwe bora zaidi.

Mhe. Spika, naomba nitowe shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuisaidia wizara yangu katika kutoa ufafanuzi kwenye mambo mbali mbali yaliyokuwa yamewapa wasi wasi wajumbe na kwa kweli wamefanya kazi kubwa isiyokuwa na mfano.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwataje vinara wa kamati hii kama wafuatavyo.

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mwanasheria wa kamati

4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mussa Khamis Silima	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
8.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
9.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
10.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu

Mhe. Spika, mswada huu umechangiwa na wajumbe 24 ukianzwa na Mwenyekiti kama nilivyomtaja;

1. Mhe. Ali Abdalla Ali
2. Mhe. Salmin Awadh Salmin
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Omar Ali Shehe
5. Mhe. Assa Othman Hamad
6. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
7. Mhe. Hija Hassan Hija
8. Mhe. Ali Salum Haji
9. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
10. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman
12. Mhe. Saleh Nassor Juma
13. Mhe. Subeit Khamis Fakih
14. Mhe. Mohammed Haji Khalid
15. Mhe. Mohammed Said Mohammed
16. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
17. Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
18. Mhe. Waziri wa Afya
19. Mhe. Fatma Mbarouk Said
20. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
21. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo
22. Mhe. Mussa Ali Hassan
23. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na
24. Mhe. Mwanasheria Mkuu

Mhe. Spika, napenda nitowe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wote hawa ambao wameuchangia mswada huu. Ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wameuchangia mswada huu kwa nia ya kuufanya uwe bora na kwa nia ya kutoa mawazo ambayo wameyapokea kutoka kwa wananchi wao, hatimaye mawaziri mbali mbali wamepata nafasi ya

kuweza kutoa ufafanuzi na kunisaidia katika kujibu hoja zao Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe baada ya ufafanuzi uliotolewa na Waheshimiwa Mawaziri, basi Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati watakuwa wameelewa madhumuni ya vifungu ambavyo vimetajwa katika mswada huu.

Mhe. Spika, kwa sababu ya kazi kubwa ambayo imefanywa ya kutoa ufafanuzi. Mimi sitofanyakazi ya kwenda kwenye vile vifungu ambavyo tayari vimetolewa ufafanuzi na Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wajumbe wengine. Hasa ufafanuzi uliotolewa na Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ujumla naomba nitambuwe kutoa ufafanuzi wa hoja 19 ambazo nahisi ni vyema nikaweza kuzitolea ufafanuzi. Nitawaomba radhi Waheshimiwa Wajumbe kwamba sitowataja kila mmoja na hoja yake, lakini nitataja makundi ya Waheshimiwa Wajumbe ambao wametoa hoja ambazo zinafanana.

Mhe. Spika, hoja ya kwanza ilikuwa ni ya ukubwa wa madaraka ya Katibu Mkuu Kiongozi. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Hija Hassan, Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Saleh Nassor Juma na Mhe. Subeit Khamis Faki.

Mhe. Spika, kimsingi ufafanuzi wa hoja hii umeshatolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuuwa Serikali, pamoja na waheshimiwa wengine wajumbe waliotangulia kusaidia kutoa ufafanuzi huo.

Lakini Mhe. Spika, kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe naomba niseme yafuatayo. Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ibara ya 49(2), Katibu Mkuu atakuwa ndiye Kiongizi wa Utumishi wa Umma kwa Zanzibar. Uongozi huwa unaambatana na dhamana. Aidha, Katibu Mkuu Kiongozi ni kiungo kati ya Mhe. Rais na watumishi wa umma.

Mhe. Spika, Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala ilipitia majukumu yake kwa kuzingatia madaraka iliyopewa ndani ya katiba na kufanya marekebisho mengi na muhimu. Kwa sasa madaraka na majukumu aliyonayo yana uwiano mzuri kati yake na vyombo vyengine vilivyopewa majukumu chini ya sheria hii.

Mhe. Spika, ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe kuwa Katibu Mkuu Kiongozi ni taasisi, kwa maana ya kuwa kuna vyombo vinavyofanya kazi kumshauri Katibu Mkuu Kiongozi, isihesabike kama ni mtu mmoja anayejiamulia mambo yake pake yake. Lakini Katibu Mkuu Kiongozi anapata ushauri kutoka kwenye taasisi ambazo anazisimamia.

Hoja ya pili Mhe. Spika, ilikuwa ni maana ya utumishi wa umma. Hoja hii hasa ilizungumziwa na ndugu yangu Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chake Chake, Mhe. Omar Ali Shehe. Mhe. Spika, Utumishi wa Umma maana yake katika sheria hii ni watu wote ambao wamepewa jukumu la kuwahudumia wananchi na ambao ajira zao ziko chini ya tume zilizotajwa katika mswada huu. Mashirika na Taasisi za Serikali pamoja na Serikali za Mitaa.

Mhe. Abubakar Khamis ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria nafikiri na Mhe. Mwanasheria Mkuu walilieleza vizuri jambo hili. Watu wanafananisha utaumishi serikalini na utumishi wa umma. Utumishi wa umma maana yake ni watumishi wote waliomo katika mihimili yote ya nchi na hawa wote wanawatumikia wananchi, kwa maana hiyo wanautumikia umma.

Hoja ya tatu Mhe. Spika, ilikuwa ni tafsiri ya afisa. Mhe. Abdalla Juma angependa kujua tafsiri iliyowekwa kwenye sheria hii maana yake ni nini. Afisa maana yake ni kila mtumishi aliyeajiriwa katika utumishi wa umma, cheo na wadhifa maana yake ni kazi anayoifanya kama ni Mkurugenzi, Ualimu, Mlinzi au Tarishi na kadhalika.

Katika muundo wa utumishi kila nafasi inatambuliwa na inawekewa majukumu na maslahi na mfumo wa kuripoti na kupimwa utendaji wake. Afisa haikusudiwi madaraka makubwa peke yake kama anavyozani Mhe. Mjumbe.

Hoja ya nne Mhe. Spika, ilikuwa ni maana ya kustaafishwa kwa maslahi ya umma na matokeo yake. Hoja hii Mhe. Mwanasheria Mkuu ameikubali kwamba tuiwekee tafsiri. Hoja hii ilichangiwa na Waheshimiwa Wajumbe watatu. Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Makame Mshimba na Mhe. Omar Ali Shehe.

Mhe. Spika, kustaafishwa kwa manufaa ya umma ni utaratibu wa kuwaondoa wafanyakazi katika utumishi wa umma kabla ya kufikia muda wa kustaafu kwa sababu mbali mbali zikiwemo za kupunguza wafanyakazi waliozidi, wafanyakazi wanaohatarisha usalama au hadhi ya chombo anachokitumikia.

Mhe. Spika, wanaostaafishwa kwa maslahi ya umma, hulipwa maslahi yao yote wanayostahiki, na wakati mwengine hupata hata zaidi ikiwa ni tunzo maalum kwa kukatisha muda wa utumishi wake.

Mhe. Spika, hoja ya tano ilikuwa ni sera ya utumishi wa umma. Hoja hii ilizungumziwa na Waheshimiwa Wajumbe wanne. Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Omar Ali Shehe na Mhe. Rashid Seif Suleiman.

Mhe. Spika, sera ya utumishi wa umma ipo tayari na imeshaidhinishwa na serikali kama taratibu na kanuni zinavyoelekeza. Tunasikitika kuwa hatujawapatia sera hiyo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wa sasa.

Mhe. Spika, ninachoweza kuwaahidi kwa niaba ya wizara yangu kwamba mara tu nitakapomaliza kuwasilisha na kupitishwa kwa mswada huu, nitahakikisha nakala za kutosha zinatolewa na Waheshimiwa Wajumbe wanapata nakala hizo. Kwa nini iwe hivi, kwa sababu kama tunavyokumbuka kwenye kipindi kilichopita, serikali ilileta kauli na Baraza hili likaridhia kwamba sera sasa itakuwa ni mali ya serikali, zitatungwa na serikali na zitaamuliwa na serikali. Isipokuwa kwa faida ya wajumbe, kwa sababu wao ndio wanaotunga sheria, sera hizo itakuwa ni vizuri zaidi nakala za sera hizo zikaletwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Jambo hili Mhe. Spika, napenda niliahidi Baraza lako tukufu kwamba tutahakikisha tunawapatia nakala za kutosha Waheshimiwa Wajumbe.

Hoja ya sita Mhe. Spika, ilikuwa ni suala la kuondolewa kwa kifungu cha 6, kinachohusu mahusiano ya utumishi wa umma na utumishi wa kisiasa. Mhe. Abubakar Khamis ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Mwanasheria Mkuu, walikieleza vizuri sana, sidhani kama mimi pamoja na kwamba ninayo majibu, sidhani kama kuna haja ya kufanya hivyo. Kwa kuokoa muda basi naomba majibu ya Mhe. Mwanasheria Mkuu yawe yametosha.

Hoja ya saba Mhe. Spika, ilikuwa inahusu watumishi wasiotaka kwenda likizo. Hoja hii ilizungumziwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin. Kwanza napenda nimpongeze sana Mhe. Mjumbe kwa umahiri wake wa kuliona hili. Mhe. Spika, ni kweli kuna watumishi ambao hawaendi likizo. Utaratibu wa sasa ni kuwa baada ya muda fulani kama hukwenda likizo bila ya sababu zilizokubaliwa na muajiri, basi likizo hiyo huwa inaruka, yaani inafutwa. Katika kanuni mpya kwa kuzingatia maoni ya mjumbe ya kwenda likizo, itakuwa ni lazima. Kwa kanuni mpya zitaweka utaratibu wa watu kwenda likizo na maana ya kuwachunguza wale ambao hawataki kwenda likizo, kwa nini hatataki kwenda likizo.

Mhe. Spika, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu, kwamba serikali itaweka kanuni ambazo zitamuwezesha muajiri kumchunguza mfanyakazi kwa nini hataki kwenda likizo. *(Makofi)*

Hoja ya nane Mhe. Spika ni kuwahusisha wananchi na wadau katika kuandaa mswada. Kwa kweli hoja hii nayo ilipata wachangiaji watano, Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Utawala) ambaye alitushauri, kwamba ni vyema mara nyengine likafanyika hili. Vile vile hoja hii ilichangiwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Spika, kwa utaratibu kinachopaswa kujadiliwa na wadau ni sera baada ya kukubalika sera hiyo kutungiwa mswada wa sheria na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Wadau walihusishwa kikamilifu katika uandaaji wa sera na sera hiyo ndiyo iliyotumika kuandaa mswada huu, kwa sababu mswada kabla ya kuwa sheria unapaswa kujadiliwa na Wawakilishi ambao ndio Wawakilishi wa wananchi.

Kwa hivyo, naamini Waheshimiwa Wajumbe wamejadiliana na wananchi wao majimboni ndio maana wakapata nafasi ya kuuchangia mswada huu.

Katika kushirikisha wadau kuna namna nyingi na namna kubwa inayokubalika ni hii ya kuwashirikisha wawakilishi wa wananchi ambao wao hupata muda wa kwenda kukaa na wananchi wao.

Lakini nataka nisema kwa zile taasisi ambazo hata kwangu zilipata kuleta barua ya malalamiko na kuelekeza mambo fulani. Kutokana na hali hiyo, nataka niwahakikishie kwamba baadhi ya yale mambo mengi yaliyokuwemo kwenye waraka wao yamezingatiwa kama alivyosema Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala) wakati walipokuwa wakifanya marekebisho juu ya mswada huu.

Mhe. Spika, nataka nikuhakikishie kuwa Serikali ya Awamu ya Saba inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein itaendelea kuwashirikisha watu mbali mbali katika kupanga na kutunga sheria. Kwa mfano, mimi binafsi nilipoingia afisini pale, basi Viongozi hawa wa ZATUK nilikaa nao na kuzungumza pamoja na kukubaliana. Sasa pengine inawezekana kwa hofu walikuwa wakiona yale ambayo walionipa ndio maana wakaendelea kutafuta ushiriki mpana zaidi wa kuweza kukubalika maoni yao.

Mhe. Spika, hoja ya tisa ni kuhusu Bodi za Wakurugenzi kumaliza muda bila ya kuteuliwa nyengine na hoja hii ilichangiwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman.

Kwa kweli suala hili limeekewa utaratibu ndani ya Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya mwaka 2002 na Sheria ya kuanzisha Mashirika au Bodi hizo.

Kwa upande wetu kama wasimamizi wa utawala bora tutahakikisha kuwa sheria zilizopo zinafuatwa, ili bodi hizo zinazomaliza muda ziweze kuundwa bodi mpya na ziweze kutimiza majukumu yao.

Hoja ya kumi Mhe. Spika, ilikuwa ni kifungu cha kumi cha kuunda tume. Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wanaona kifungu hiki kifutwe na hoja hii ilichangiwa na Mhe. Omar Ali Shehe na Mhe. Rashid Seif Suleiman. Kwa kweli kifungu hiki ndio muhimili mkuu wa usimamizi wa sheria hii, yaani ndicho kilichoweka majukumu ya tume zilizopo na ikibidi kuanzishwa tume nyengine kama Mhe. Rais atakavyoona inafaa, bila ya kifungu hiki uzito wa sheria hii utakuwa haupo.

Aidha kifungu hiki kimeweka misingi ya taasisi zinazojitegemea ambazo zinatoa huduma kwa wananchi. Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Mjumbe aliyetoa hoja hii ninamuomba akubaliana nasi kwamba kifungu hiki bado kiendelee kuwepo.

Hoja ya kumi na moja muda wa kukaimu uainishwe na hoja hii ilichangiwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman. Kwa maana hiyo, muda wa kukaimu kwa sasa ni mwaka mmoja, lakini baada ya kupitishwa mswada huu tunategemea kuweka kanuni bora zaidi za kukaimu pamoja na maslahi ya kukaimu.

Vile vile hoja ya kumi na mbili fursa ya kuajiriwa wafanyakazi kutoka sehemu zote na hoja hii ilichangiwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyewizara Maalum). Kwanza wao walipongeza kuwepo kwa hiki kifungu, yaani sheria imeweka uwazi zaidi katika ajira, ambapo nafasi za ajira zitatangazwa na ubaguzi wa aina yoyote kwa watu wanaostahiki hauruhusiwi, bali ushindani wa sifa ndio utakaofanyakazi zaidi. *(Makofi)*

Hoja ya kumi na tatu madaraja ya wafanyakazi na hoja hii ilichangiwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman na Mhe. Mohammed Haji Khalid. Suala hili limezingatiwa katika mswada huu na hii ni moja kati ya kazi za Tume za Utumishi, yaani zile Tume za Utumishi kwa sasa Tume ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Mahakama, Tume ya Utumishi Serikalini pamoja na Tume ya Idara Maalum, itazingatia kukifanyiakazi kifungu hiki.

Hoja ya kumi na nne Mhe. Spika ni kuhusu wafanyakazi wapewe mkataba wa kazi na hoja hii ilichangiwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman na Mhe. Mohammed Haji Khalid. Wafanyakazi wote kabla ya kuajiriwa hujazishwa

mkataba na mswada huu umeweka wazi kuwa kila mwajiriwa awe na mkataba kama ilivyo katika vifungu vya 60 na 61 na hasa 61 (2).

Mhe. Spika, hoja ya kumi na tano kuhusu kuendelea kuajiri wastaafu na hoja hii ilichangiwa na Mhe. Assaa Othman Hamad, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Mussa Ali Hassan. Kwa kweli kuwaajiri kwa muda wastaafu kunafanyika pale tu ambapo hajapatikana mtu mwenye uwezo bora wa kujaza nafasi hiyo, lakini ni utaratibu wa nchi nyingi duniani huwatumia watu wenye vipaji maalum na uzoefu katika kila fani. Hali hii ina lengo la kuhakikisha kuwa wanafikia kiwango cha juu katika ufanisi na ugunduzi.

Lakini pale ambapo vigezo vilivyotajwa hapa havitokuwepo wala haja ya kufanya hivyo itakuwa haipo, basi wizara yangu pamoja na serikali kwa jumla itahakikisha haajiriwi mtu kazi hata yule ambaye hana umuhimu na vigezo ambavyo vimetajwa hapa. *(Makofi)*

Hoja ya kumi na sita ni kuhusu maslahi ya wafanyakazi na muundo wa utumishi na hoja hii ilichangiwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Assaa Othman Hamad, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mhe. Spika, maslahi ya wafanyakazi yameekewa utaratibu na ni moja kati ya Wizara, Tume pamoja na Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Nikiendelea kufanya majumuisho sasa niende kwenye hoja ya kumi na saba kuhusu utitiri wa vyombo vinavyosimamia ufanisi na hoja hii ilichangiwa na Mhe. Saleh Nassor Juma. Kwa kweli kila chombo kinachoundwa kinachukua jukumu la kutoa huduma kwa wananchi katika sekta husika. Hata hivyo, sheria hii imeweka utaratibu wa kuunda taasisi hasa katika sehemu nne ya kifungu cha 50 hadi 55 kutakuwa na utaratibu wa kufanya mapitio kama ilivyo kifungu cha 44.

Mhe. Spika, kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe mimi sijaona kama kuna utitiri wa vyombo, kwa sababu vyombo vilivyotajwa hapa kwenye sheria hii ni Kamisheni ya Utumishi Serikalini au Kamisheni ya Utumishi wa Umma ndio itakayokuwa *regulator* wa zile tume nyengine, yaani ni sawa na Benki Kuu na benki nyengine za biashara. Kwa hivyo, kazi yao ni Kamisheni ya Utumishi wa Umma ni ku-*regulate* zile sheria zinazotawala katika tume nyengine.

Sasa tukisema tunapunguza utitiri wa tume hizi hoja itarudi pale pale, kwamba sasa wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi watakuwa wakiamuliwa pengine na Tume ya Utumishi Serikalini. Pia wafanyakazi wa Mahakama watakuwa wanaamuliwa na Tume ya Utumishi Serikalini vile vile na wafanyakazi wa Idara Maalum watakuwa wanaamuliwa na Tume ya Utumishi Serikalini.

Kutokana na hali hiyo, maoni yangu, ya serikali pamoja na madhumuni ya mswada huu sioni kwamba kuna utitiri wa taasisi ambazo zinaongoza au zinasimamia shughuli hizi.

Mhe. Spika, hoja ya kumi na nane ni fursa ya migomo na hoja hii imechangiea na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Saleh Nassor Juma na Mhe. Subeit Khamis Faki. Kwa kweli migomo sio njia bora ya kutatua matatizo, kwani kuwaathiri wananchi wanaotegemea huduma kutoka vyombo vya umma.

Kwa mfano, tumekuwa tukisikia athari mbali mbali zinazowapata wananchi ikiwa ni pamoja na vifo kwa watu wanaohitaji huduma za haraka. Imani yangu kuwa vyombo mbali mbali vya kutatua migogoro ya kazi pamoja na vyombo kama chetu cha Baraza la Wawakilishi, nadhani hatutashindwa kutatua matatizo yetu hadi kufikia hatua ya kugoma na kuwaumiza wapiga kura wetu.

Aidha niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kuwa tukishadidia migomo athari si kwa muajiri pekee, bali ni kwa jamii nzima na taifa kwa jumla. Hata hivyo, utaratibu wa mgomo umo katika Sheria ya Mahusiano Kazini Nam. 1 ya mwaka 2005 kifungu cha 63 (1) na kwa upande wa mswada huu tumeweka njia bora ya kutatua matatizo kwa watumishi wa umma, ili tusifikie katika hatua ya kugoma, jambo ambalo pia ni aibu kwa nchi yetu na aibu kwa nchi yenye kuendesha mambo yake kwa mujibu wa Sheria na Katiba hasa kwa Zanzibar ambayo sasa tumejikita katika kufuata utaratibu au misingi ya utawala bora. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hoja ya mwisho ambayo ni ya kumi na tisa inayohusu uwiano wa wanawake, wanaume na waathirika wa UKIMWI, hoja hii ilichangiwa na mchangiaji mmoja ambaye ni Mhe. Fatma Mbarouk Said. Madhumuni ya kifungu hiki ni kuondosha ubaguzi wa kijinsia katika ajira pia kifungu hiki kinataka kuwe na uwiano uliobora wa wanawake na wanaume katika ajira.

Aidha kinazuia unyanyapaa ambao unaweza kujitokeza katika ajira na kukataza waajiri wasiwanyime haki ya kuwaajiri watu walioathirika na UKIMWI. Vile vile kifungu hiki kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo jana kwamba kinatilia mkazo namna ya kuwapa au kuwatendea haki ndugu zetu watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ni imani yangu Waheshimiwa Wajumbe watakubaliana na ufafanuzi ambao umetolewa na Waheshimiwa mbali mbali wakiwemo Mawaziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na ule nilioutoa mimi hivi sasa.

Kwa hivyo, naomba kutoa hoja Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa. Sasa niwahoji wale wanaoafiki hoja ya Mhe. Waziri juu ya mswada huu wanyanyue mikono, wasioafiki, walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya 2011, Zanzibar

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya 2011, Zanzibar

Kifungu cha 1	-	Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu cha 2	-	Matumizi ya Sheria pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 3	-	Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 4	-	Misingi mikuu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 5	-	Maadili makuu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 6	-	

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya serikali kuanzia Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wenyewe. Lakini kwa sababu Mhe. Mwanasheria Mkuu amekiri mwezi wa nne tunategemea kupata mswada unaohusu maadili ya Viongozi hasa wa Kisiasa na kwa sababu mswada huu umezungumzia hasa Utumishi wa Umma na Katiba inasema wazi kwamba Utumishi wa Kisiasa si Utumishi wa Umma.

Kwa hivyo, ninaomba serikali ikubaliane nasi kwamba kifungu cha 6 kiondolewe na tusubiri mwezi wa nne kwa ajili ya kujadili mswada unaohusu suala hili kwa upana zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kama maelezo yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa kweli kifungu hiki kinaweka uhusiano tu na wala si jambo jengine, sio kwamba kuwepo kwa kifungu hiki kunafanya sasa utumishi wa siasa unasimamiwa na utumishi wa umma,

isipokuwa ni uhusiano kama alivyofafanua zaidi Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo, Utumishi wa Kisiasa unategemeana na mambo mengi yanayoendeshwa katika nchi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe atukubalie kwamba kifungu hiki kiendelee kubali, kwani hakina madhara yoyote kuwepo hapa, lakini itakuwa ni tatizo kama kifungu hiki kitaondoka, kwa sababu kinazungumzia zaidi masuala ya uhusiano.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi si mwanasheria, lakini ninavyoamini uhusiano kwa jumla umetandikwa vizuri kwenye Katiba ya Zanzibar, kwa kweli Katiba ya Zanzibar haikuacha kitu, yaani imezungumza mambo yote yanayohusu uhusiano na maadili ya kila jambo. Kutokana na hali hiyo, wasiwasi wangu ni kwamba mswada huu wa sheria ukipita leo maana yake Katibu Mkuu Kiongozi sasa asimamie maadili hata ya watumishi wa umma pamoja na viongozi watumishi wa kisiasa, jambo ambalo Kikatiba halimo kwenye utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa sheria ya dini inatwambia jambo likiwa na wasiwasi basi ni vyema kuliacha. Sasa busara za Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba mwezi wa nne kuna mswada unakuja kuhusu watumishi wa kisiasa, basi ningemuomba kwa hisani yake akatuachia mwezi wa nne tukapata kujipanga pamoja na kutafuta mawazo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, anachoeleza Mhe. Hija Hassan Hija kidogo ni tofauti na maudhui yaliomo kwenye kifungu cha 6. Kwa kweli kifungu hiki kinaelezea uhusiano wa utumishi, kwa maana kwamba watumishi hawa wa kisiasa na umma ni watu ambao wamo katika serikali. Sasa ikiwa wamo kwenye serikali basi lazima kuwe na mahusiano fulani ambayo kwa pamoja ndio hiyo serikali itaendeshwa.

Kwa hivyo, kifungu hiki kinasema ihakikishe kuna sheria maalum, hapa inatoa agizo kuwa lazima kuwe na sheria maalum ambayo itatungwa yenye kuzungumzia suala la utumishi wa kisiasa.

Vile vile ni lazima kujua katika utumishi ikiwa wa kisiasa au umma, unapoingia kwenye utumishi basi lazima ujue ni kitu gani ambacho unatakiwa wewe kama mtumishi ulioingia pale unatakiwa ufanye. Kwa hiyo, haya ni maagizo ya kifungu hicho cha kuelezea kwamba anapoingia mtumishi wa kisiasa awe na maelekezo haya na yule wa umma awe na maelekezo yale.

Kwa maana hiyo, hiki ni kifungu ambacho kinaelezea tu, namna gani kinachotakiwa kiwe na wala hakihusiani na utendaji wa kazi au Katibu Mkuu Kiongozi atawaingilia hawa wanasiasa, kifungu hiki hakielezei hivyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naendelea kukiri kwamba mimi si mwanasheria, isipokuwa ninasoma Katiba inasema kwamba kifungu cha 134 (2) kinasema wazi kwamba, kwa sababu ya utumishi wa kisiasa si utumishi wa umma pale ambapo panahitajika kufanya hivyo, Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

> Kifungu cha 134 (2) cha Katiba ya Zanzibar kinasema hivi:-
>
> "Ila iwapo maelezo yanahitajika vyenginevyo, uwezo wowote uliopewa Baraza la Wawakilishi na Katiba hii kwa kuanzisha au kuendeleza jambo lolote, basi utafanywa kwa kutungwa sheria".

Mhe. Mwenyekiti, naomba tukubaliane na mawazo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwamba tusubiri mswada wa sheria mwezi wa Aprili kwa ajili ya kujadili kwa upana zaidi juu ya suala hili na huu ni mswada wa Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 134 (2) cha Katiba ya Zanzibar naomba kunukuu.

> Kifungu cha 134 (2) cha Katiba ya Zanzibar kinasema hivi:-
>
> "Ila iwapo maelezo yanahitaji vyenginevyo, uwezo wowote uliopewa Baraza la Wawakilishi na Katiba hii kwa kuanzisha au kuelezea jambo lolote, basi utafanywa kwa kutungwa sheria".

Mhe. Mwenyekiti, hapa tunazungumzia uwezo uliopewa Baraza la Wawakilishi ni tofauti na hiki kifungu ambacho kinasema au kinaagiza itungwe sheria, yaani haya ni maagizo mengine, isipokuwa hapa ni uwezo wa Baraza la Wawakilishi na wala hapa hatuzungumzii uwezo wa Baraza la Wawakilishi, kwa sababu uwezo wa Baraza upo wakati wowote ule.

Lakini haya ni maagizo mengine ambayo tumepewa kwenye mswada huu, maagizo hayo ndio yatakayotufanya sisi tutunge hiyo sheria ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu aliyosema. Kwa hivyo, hivi ni vifungu viwili tofauti ambavyo vinaelekeza mambo mawili tofauti.

Kwa maana hiyo, bado kifungu cha 6 kina umuhimu wake kuwepo kuonesha kwamba uhusiano huu wa kisiasa na utumishi wa umma ni lazima uwepo. Sasa utumishi wa kisiasa lazima uwepo katika sheria ambayo itatungwa. Kwa hivyo, tukiondoa hiki tunaondoa ule uwezo wa kuweka sheria ya utumishi wa kisiasa, kwa sababu itakuwa hakuna maagizo mengine, kwani maagizo yaliomo humu ni maagizo ambayo tumepewa Baraza la Wawakilishi kwa kutunga sheria ambayo tunahisi tunaweza kuitunga kwa shughuli nyengine. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi namfahamu sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kwa sababu mimi pengine si mwanasheria nitakuwa sina uwezo wa kubishana nae, ningeomba Baraza liamue kupiga kura na nikishindwa nitaridhia.

Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti mimi sina maelezo ya ziada kifungu ni muhimu kuwepo na hakizungumzii hivyo ambavyo Mhe. Mjumbe amedai, kwa hivyo kama Baraza lako linaamua twende kwenye kura ni demokrasia. Lakini serikali bado inaona kifungu hichi ni muhimu kuwepo.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri kabla hatujaamua kwenda kwenye kura kwa umuhimu au mantiki aliyozungumzia Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, basi nilikuwa na rai mimi ya kufanya kwamba hiki kifungu cha sita kiendelee kubaki mpaka kifungu kidogo cha pili (a) lakini (b) na (c) zitolewe.

Mhe. Spika: Kumekuwa na mashauri hayo kwamba anakubali kifungu hiki katika kuunga mkono hoja pale kibaki kama kuungwa mkono hoja ya serikali, lakini (b) na (c) iondoke.

Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, bado mimi nakuwa mgumu na sababu zangu ni hizi, kwa mfano hiki kifungu cha (b) kinasomeka kuweka utumishi chini ya mapitio ya kawaida kwa ajili ya kuhakikisha kuwa malipo, mafao na maslahi yanalingana na utumishi wa umma. Sasa kilichokusudiwa hapa ni kwamba sisi sote hapa ni wanasiasa na ndio watumishi wa kisiasa na sisi kamati ya uongozi inapoamua mafao na maslahi yetu tunakwenda wapi, tunakwenda serikalini. Sasa sioni sababu ya tatizo hili kwa hivyo mimi bado nahisi kifungu hiki hata Mheshimiwa alivyopendekeza kibaki nahisi kibakie.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa maana hiyo sasa inaonekana twende kwenye kura juu ya suala la kifungu kubaki au kukiondoa.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi Mipango na Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kuna haja ya kufahamu kwa kina kinachozungumzwa hapa ni utumishi wa umma sio utumishi wa serikali, na utumishi wa umma kama ilivyofafanuliwa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwamba pila zote tatu zimo ndani. Lakini Mwenyesheria Mkuu alinitolea mfano mimi, alimtolea mfano Dr. Mwinyihaji, sisi tulikuweko huko serikalini na baadae tukatoka tukenda katika siasa sheria gani ambayo inatuunganisha hapa, ndio Waziri anasema kwamba hiki kifungu kiwepo kuruhusu kuweka hiyo sheria vyenginevyo utakuwa huna kifungu cha kumruhusu mtumishi wa umma kuweka hiyo sheria na sheria yenyewe ndio hii hii.

Katika hiyo Sheria huo uhusiano ambao Mhe. Waziri anauzungumza una-*relate* na hivi vifungu (b) na kifungu cha (c) ambao Mwanasheria ameuzungumzia hapa uhusiano wetu wa mishahara, leo nikiwauliza waheshimiwa wawakilishi hapa wao wana viinua mgongo wana pencheni, uhusiano wao na utumishi mwengine ukoje. Haya ndio ambayo tunasema sisi hivi vifungu vibakie ili tuende katika hiyo sheria ambayo itatuchanganulia haya (a) (b) na (c).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kifungu hiki tukikubali kiendelee lakini kama Waheshimiwa Wawakilshi wanataka lazima tupige kura basi na mimi nasema kama alivyosema Mhe. Waziri, lakini na mimi nasema kwamba kuna umuhimu wa kifungu hiki kuendelea nacho.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika watu waliotaka kifungu hiki kitolewa mimi ni mmoja wapo niliyeanza kujenga hoja hiyo, kwa sababu pamoja na maelezo ambayo yametolewa na wanasheria juu ya utumishi wa umma na utumishi wa kisiasa, ukiangalia katiba yetu hii ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo 2010. Ibara ya 134 ukiangalia juu ya tafsiri ya utumishi wa Umma imewatoa kabisa watumishi wa kisiasa na inaonyesha kwamba hakuna uhusiano wowote kati ya utumishi wa umma na utumishi wa kisiasa.

Mhe. Mwenyekiti, uhusiano ambao Mwanasheria ameuzungumza hapa ni uhusiano wa kawaida tu ni sawa sawa na kusema kuna uhusiano kati ya binaadamu na wanyama, kwa sababu wanyama tunawafuga ng'ombe, simba tunawafuga uhusiano upo. Lakini Mhe. Mwanasheria aliposema kuna uhusiano na akatoa tafsiri kwamba tuna uhusiano katika mambo yetu, sheria tunapozitunga lazima ziende kwa Mhe. Rais kwa hivyo huo ni uhusiano wa kawaida, lakini katika yetu imeutoa kabisa uhusiano wa utumishi wa umma na utumishi wa kisiasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa misingi hiyo mimi nakubaliana na hoja kwamba kifungu hiki kitoke kwa sababu hakina maana yoyote katika suala hili, pengine kifungu kinachozungumzia 6 (b) mbali na uhusiano huo wa utumishi wa kisiasa kinazungumzia zaidi kuweka utumishi chini ya mapitio ya kawaida kwa ajili ya kuharakisha kuwa malipo, mafao na maslahi ya wanasiasa yanalingana na ya utumishi wa umma.

Lakini kifungu cha 6 (c) kinazungumzia kupitia malipo kuyapitia maana yake, haya maslahi tunayoyapata kuyapitia malipo na mafao ya wastaafu na maposho mengine ya viongozi wa kisiasa, kwa hivyo hakuna muingiliano katika sehemu hizi kwa mujibu wa katiba na kwa mujibu wa maslahi. Kwa hivyo tunaomba suala la uhusiano kati ya vyombo hivi ni jambo la kawaida upo sisi tunaelewa kwamba tuna uhusiano kwa sababu sisi sote tunawatumikia wananchi, lakini katika kuhakikisha kwamba kuna jambo hili la uhusiano la kutungiwa sheria nadhani kama kuna haja ya serikali kutunga sheria hailazimishi.

Mhe. Mwenyekiti, wewe unafahamu kwamba serikali inapokuwa na haja au hoja ya kutaka kutunga sheria hailazimishwi na sheria nyengine, sheria hii inalazimisha kutungwa kwa sheria, Katiba peke yake ndio inayoshawishi au kutoa maelekezo ya kutungwa sheria juu ya utekelezaji wa jambo fulani. Sheria huwa inalazimisha kuundwa kanuni juu ya utekelezaji wa jambo fulani, ni katiba peke yake inayoruhusu au inayoshawishi kutungwa sheria kwa ajili ya utekelezaji wa katiba hii.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Kuna mashauriano kidogo hapo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti baada ya kushauriana na Kiongozi wa serikali katika Baraza la wawakilishi tunakubali tufuate ushauri wa Mhe. Abdalla Juma aliosema kwamba ile kifungu cha 6 (b) na (c) tukifute na vile vyengine vibakie. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Hoja hasa ni Mhe. Hija Hassan, sasa unasemaje baada ya makubaliano haya.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hizo ni busara za viongozi watu wazima nakubali tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti kwa maadhumuni ya uandishi bora tunasema tunaipitisha kama sheria ya kupitisha vifungu ina maana tena kifungu cha pili hakina a na b tena kwa hivyo ningependekeza ili kisomeke vizuri kikasema. Katika kusimamia uhusiano unaotajwa kutoka kijifungu cha

kwanza cha kifungu hiki kutapitishwa sheria maalum ya usimamizi wa kisiasa na kwamba sheria hiyo itatungwa na kuonyesha kiwango kinachotakiwa kwa ajili ya ufanisi, au ubora wa utumishi wa kisiasa napendekeza kama kawaida tu.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri tunakubaliana na mawazo aliyoyatoa na tunaendelea kwa kufanya marekebisho tuliyokubaliana hapa.

Kifungu cha	6	-	Uhusiano wa Umma pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha	7	-	Kanuni za maadili ya utumishi wa umma
Kifungu cah	8	-	Maadili ya kitaaluma pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha	9	-	Utakelezaji wa kanuni za Maadili pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha	10	-	Muundo wa Utumishi wa Umma pamojana Marebisho Yake
Kifungu cha	11	-	Usimamizi Mkuu na uongozi wa jumla pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha	12	-	Mamlaka ya uteuzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha	13	-	Kutekeleza majukumu pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni makosa ya uchapaji lakini ni vizuri tukaweza kurekebisha, ule mstari wa pili kutekeleza yoyote ukiweka yote inabadilisha kabisa maana iliyokusudiwa nadhani isomeke yoyote. Rais anaweza kutangaza kwa tangazo litakalochapishwa na serikali kwenye gazeti rasmi kuagiza kutekeleza yoyote katika majukumu yafuatayo. Lakini ukisema nitaagiza majukumu yake yote tana hap Rais atakuwa hana kazi tena.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, waheshimiwa tufanyeni marekebisho iwe yoyote na sio yote.

Kifungu cha 13 - Kutekeleza majukumu pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 14 -

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti pamoja na maelezo yote niliyoelezwa lakini bado mimi kichwa changu hakijashawishika, kuwa Katibu Mkuu Kiongozi wakati amashastaafu apewe malipo yote bado nashawishika ni

kweli viongozi wetu tuwaenzi lakini apunguziwe asipewe mshahara wote, bado na sema bado kwa sababu anaweza kuwa yeye sasa hivi kuwa katibu mkuu kiongozi sawa sawa.

Baadae anakuja mwengine yeye hayupo tena, halafu anakuja mwengine na kila atakayekuja atapewa mshahara kamili, wakifika watu kumi serikali itafilisika, kwa hivyo naomba hili liangaliwe bado mimi sijashawishika.

Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kidogo kuna tofauti ya maelezo ya Mhe. Mjumbe inaonekana mtazamo wetu ni kwamba mafao ambayo atalipwa Katibu Mkuu kiongozi kama ni ya kutunzwa, kama anavyotunzwa Mhe. Rais, anavyotunzwa Jaji Mkuu, Spika, hii kidogo nafikiri ni tofauti. Katibu Mkuu kiongozi inazungumzia pale anapotoka kwenye nafasi yake ya ukatibu mkuu kiongozi, lakini hajastaafu analipwa mafao yake yale yale. Kwasababu bado anakuwa ni mtumishi wa serikali.

Kifungu chengine kinaelezea Katibu Mkuu kiongozi atakapokuwa amestaafu atalipwa mafao kulingana na mafao anayolipwa Katibu Mkuu Kiongozi aliyopo, sasa mafao haya sio yale ya kutunzwa ni mafao ambayo anahesabiwa kama vile anavyohesabiwa mfanyakazi mwengine yoyote yule ambae amemaliza muda wake, kwa hivyo kwenye ile sheria inawahusu viongizo wastaafu kuna tofauti na kifungu hiki. Yaani maelezo ya kifungu hiki yanatofautiana kabisa na mawazo ambayo pengine Mhe. Mjumbe ameyatoa au labda niwe sijamfahamu.

Mhe. Subeit Khams Faki: Mhe. Mwenyekiti, kifungu kinasema wakati wa kustaafu atapata mafao yake Katibu Mkuu Kiongozi aliyepo pale madarakani.

Mhe. Mwenasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti kifungu kipi anachokisema kwa sababu hatujakijua.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Hiki ni kifungu cha 14.6 kuna (a) (b) na (c) ndio ninavyosema wakati ameshastaafu asilipwe mshahara kamili.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo unachokihoji hasa ni kfungu (b) kwamba atalipwa sio chini ya kiwango cha mshahara wa Katibu Mkuu Kiongozi aliyopo.

Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, labda atwambie anapendekeza nini.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa unapendekeza nini.

Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti mimi nashauri basi au nakubali kwamba kuondosha ile asilimia mia moja na tufuate mfano mwengine wa kitaifa, apata asilimia thamanini ya mshahara wa Katibu Mkuu Kiongozi aliyopo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti apewe nusu ya asilimia hamsini asipewe asilimia thamanini, lakini apewe asilimia hamsini.

Mhe. Mwenyekiti: Labda hapa niseme maneno kidogo unajua jambo hili lilikuwepo kwa viongozi wakuu wa kisiasa na tulipata tabu sana kumshughulikia Spika, mtaafu huyu Mzee Ali Khamis ilikuwa hatuna pa kushika, si muda mkubwa kama mwaka mmoja uliopita tukapata maelekezo rasmi kwamba utaratibu utakaotumika ni kwamba ni kama vile wanavyotumia wenzetu bara. Kiongozi mstaafu yule atapata asilimia thamanini hii anayoisema Mhe. Waziri ya mshahara wa spika aliyopo.

Sasa sina hakika kama Katibu alipokea maelezo mengine ya kubadilisha hilo, lakini katika viongozi wakuu ipo utaratibu huo kwamba atalipwa kama pencheni sio mshahata lakini pencheni ya asilimia thamanini ya mshahara wa spika aliyekuwepo madarakani hiyo inazungumzia kwa Spika, sasa anachopendekeza Mhe. Waziri hapa kwamba na kiongozi huyu mkuu wa utumishi wa umma basin a yeye angepewa kima hicho ndicho alichokuwa anasema Mhe. Waziri.

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti hapa kidogo tunaweza kujichanganya hapa kwanza huu mshahara kila mmoja na uelewa wake, maana ya mshahara kwa tafsiri yaw engine ni yale mafao yote mtu anayopata kwa mwezi. Lakini hali halisi ya mshahara sio chote tunachopata kwa mwezi, kuna basic salary pamoja na mafao mengine, sasa nadhani hapa tungelipaweka wazi kwa sababu huyu bado kwa hiki kifungu hiki bado yumo kazini, sasa tukisema tumpe asilimia thamanini, au sitini hofu yangu kwamba anaweza kuja kupata kidogo zaidi kuliko hata Makatibu Wakuu.

Sasa mimi nadhani tungebakia hii kama ilivyo kwa sababu hapa unaozungumzwa ni mshahara, bila ya shaka ikiwa yeye sio katibu Mkuu Kiongozi atakapoondoka hapa mafao ya katibu Mkuu Kiongozi mengine atakuwa hapati, sasa kwa kumuachia mshahara bado nafasi ipo kati yake na Katibu Mkuu Kiongozi kwasababu Katibu Mkuu kiongozi aliyekuwepo madarakani bado kuna mafao mengine atakuwa anapata huyu atakuwa hapati.

Mhe. Mwenyekiti: Ili tuhamiane vizuri kwa hivyo huyu bado yuko kazini lakini hashiki madaraka ya Katibu Mkuu Kiongozi ndio maana yake hiyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kusaidia hilo hilo alilosema Mhe. Haji Faki Shaali lakini labda kwa ufafanuzi zaidi, naomba tukikisoma hiki kifungu tusikisome hivi vitoto peke yake peke yake tuanze hapa kilipoanzia. Katibu Mkuu Kiongozi atashika wadhifa wake kwa ridhaa ya Rais lakini ikitokea hali ya kuondolewa kwake sio kustaafu, sio kufukuzwa lakini kuondolewa. Rais kafanya mabadiliko kama anavyofanya kwa mawaziri au anavyofanya kwa makatibu wakuu, huyu sio katibu mkuu kiongozi tana. Isipokuwa kama kuondolewa kwake ilikuwa kwa sababu ya tabia mbaya ambayo alipata fursa ya kujibu tuhuma na kutoa utetezi.

Sasa mimi nasema akiondolewa kwa nafasi hiyo hatoteuliwa kushika nafasi ya ngazi ya chini ya ukaribu mkuu, kwamba huwezi tena Katibu Kiongozi ukamfanya mkurugenzi umemuangusha angalau afike Katibu Mkuu wa kawaida, pili anapofanya hiyo kazi nyengine sasa atalipwa mshahara sio chini ya mshahara wa Katibu Mkuu Kiongozi aliyekuwepo mshahara.

La tatu wakati wa kustaafu baada ya kuwa yameshafanywa yote hayo atastahiki kupata mafao maalum ya kumalizia ambayo Katibu Mkuu kiongozi alipokuwa anastahili wakati wa kustaafu, hili nadhani ni suala la kawaida hata akistaafu alipwe mafao kama alivyowahi kushika wadhifa wa ukatibu mkuu. Kwa hivyo mimi nadhani hiki kifungu hakina matatizo na tukipitishe.

Mimi nilikuwa na langu jengine lakini sio kwa kifungu hiki na nitalisema baadae tumalizie hiki kwanza, kwa hiki cha sita naomba tukiwacheni.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tumeelewana vizuri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Mhe. Ismail Jussa Ladhu kazidi kunichanganya, sasa mtu katolewa kwa utovu wa nidhamu ndio kabisa, halafu tumpe maisha mazuri kama aliyekuwemo na wakati ameshatolewa na nafasi ile haitumikii, ndio kabisa sasa tumpe mshahara ule ule. Bado kazidi kunichanganya.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri hapa tatizo sasa ni kutokufahamu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumsaidia Mhe. Ismail Jussa Ladhu hebu tukikisoma hiki kifungu kuanzia hapo isipokuwa tusiingize, tufanye kama haipo hiyo isipokuwa. Tusome Katibu Mkuu Kiongozi atashika wadhifa wake kwa ridhaa ya Rais lakini ikitokea hali ya kuondolewa kwake hatoteuliwa kushika ngazi ya chini ya ngazi ya Katibu Mkuu, atalipwa mshahara sio chini ya kiwango cha mshahara wa katibu mkuu wakati atakapostaafu atastahiki kupata mafao maalum.

Habu hiyo ispokuwa kwanza tusiitizame ni kwamba huyu bwana kaondolewa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi kafanywa Mkuu wa Mkoa, sasa huyu angekuwa muda wake wa kustaafu ungefika angepata maslahi ya katibu Mkuu Kiongozi, lakini kaambiwa kafanye kazi nyengine na ameshaitumikia kazi ya Katibu Mkuu Kiongozi. Sasa anastaafu baada ya mwaka mmoja ndio alipwe maslahi ya Mkuu wa Mkoa jamani, yote yale aliyokaa pale kuwa Katibu Mkuu kiongozi tumeyasahau.

Sasa anasema kama kaondolewa mambo ni mengine, lakini kama hakuondolewa kwa nidhamu maslahi haya ayapate, jana nilisema hapa kwamba mimi nimeondolewa lakini mshahara unakuwa ni *hurt my selfu* ndio maana akasema jamani msimpe cheo kidogo ni udhalilishaji, hatoteuliwa kushika ngazi ya chini ya katibau mkuu kusidi kwamba ni heshima. Sasa kama atawekwa cheo chengine anapostaafu apate maslahi aliyoyafanyia kazi kama Katibu Mkuu Kiongozi, sasa mkidharau kwamba yeye hakufanya kazi ya Katibu Mkuu Kiongozi mna mnyima fursa ile.

Sisi hapa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hiki cheo ni kikubwa jamani. Nimesema hapa magavana wa Benki Kuu wanalindwa. Mkilinganisha basi huyu ndiye anayeendesha serikali. Rais ni mshauri wake tu, anasema hilo nakubali na hilo nakataa. Sasa wende ukampe mshahara nusu kwa sababu ni Mkuu wa Mkoa? Haielekei jamani. Hizi ndio taratibu za utawala sio kwamba tunazitaka sisi. Hii imewekwa kwenye sheria ili kulinda na hii ndio taratibu ya utawala wa serikali. Yeyote yule ambaye hajakosea, hajafanya utovu wa nidhamu, hajastahifishwa kwa maslahi ya umma. Kama kastaafishwa kwa maslahi ya umma ndio hii isipokuwa inaingia.

Nadhani Mheshimiwa kifungu hiki hakina dosari.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Subeit Khamis Faki, nafikiri tumejaribu kufahamishwa vizuri na mawaziri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti nimefahamu vizuri sana na unajua hili suala limeshaingiliwa na watu wazima. Sasa suala likishaingiliwa na watu wazima siku zote watoto huwa wananyweya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba hili suala tuliangalie vizuri ikiwa kaondolewa kwa utovu wa nidhamu basi mishahara kamili asipewe. Ikiwa kaondolewa kwa sababu kama hizo basi mshahara wake aendelee kupewa. Lakini naomba mwenyekiti na sisi watu wa siasa mutuangalie.

Mhe. Mwenyekiti: Naamini Mhe. Waziri tupo sahihi au kuna nyongeza.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nadhani alivyosema Mhe. Subeit ndivyo inavyosema. Kwa hiyo hakuna sababu.

Kifungu cha 14 Uteuzi na Majukumu ya Katibu Mkuu Kiongozi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nilisema pale mwanzo nilikuwa na jengine nje ya hili Mhe. Mwenyekiti. Kifungu cha 14 kifungu cha 4(b) Uandishi katika kuchapa kuna baadhi ya maneno yameachwa, sivyo ilivyokuwa imekubaliwa ndani ya Kamati. Nasema kisomeke "**Atainua uwajibikaji wa Utumishi wa Umma** " Sio wa umma. "**kwa kuelekeza kuwa na mtazamo unaozingatia misingi mikuu ya utumishi wa umma"** kama ilivyotajwa katika kifungu cha 4(i) cha sheria hii.

Imesahaulika *phrases* mbili Mwenyekiti kwanza pale mwanzo ilipoanzia "**atainua uwajibikaji wa utumishi wa umma"** sio wa umma, maana hawezi kuwajibisha umma wote huu.

Mstari wa pili **"kwa kuwelekeza kuwa na mtazamo unaozingatia misingi mikuuu ya utumishi wa umma kama ilivyotajwa katika kifungu cha 4(i) cha sheria hii.**

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri Mhe. Waziri ipo sawa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Ni sahihi.

Kifungu cha 14 Uteuzi na Majukumu ya Katibu Mkuu Kiongozi Pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliobaki hautoshi kuliwezesha Baraza kukamilisha kazi inayoendelea ya Mswada wa Sheria kabla ya muda wa kuahirisha Baraza kwa mujibu wa Kanuni. Naomba Baraza lako tukufu kuongeza muda ili kuweza kuendelea na shughuli mpaka tutakapomaliza.

Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Kifungu cha 15	Ripoti ya Mwaka ya Katibu Mkuu Kiongozi.
Kifungu cha 16	Sekretariet ya Baraza la Mapinduzi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 17	Uwanzishwaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 18	Muundo wa Kamisheni Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 19	Sifa za Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamisheni Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 20	Muwa wa Kushika Kuondolewa na Kukosa sifa kwa Mwenyekiti au Mjumbe Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 21	Uchunguzi Dhidi ya Tabia ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamisheni Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 22	Uteuzi na Kazi za Katibu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 23	Idara za Kamisheni.
Kifungu cha 24	Mikutano ya Kamisheni Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 25	Kazi za Kamisheni Pamoja na Marekebisho Yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante, Mheshimiwa ni yale yale yanayohusu lugha na uchapaji Kifungu cha 25 kwenye (M), (O) na (P)

(M) Mstari wa pili yale maneno "**katika taasisi"** Yanapaswa yaondoke kwa sababu taasisi zimeshaingizwa huku juu. **"Kupitia taratibu katika taasisi za usimamizi wa utumishi wa umma"**.

(O) Kuna neno "**Kuidhinisha Mipango ya Utumishi**" bali lisomeke Kuidhinisha Miundo ya Utumishi *(schemes of service*).

(P) neno la mwisho kabisa lisomeke Sheria nyengine yoyote sio yeyote.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Sawa.

Kifungu cha 25	Kazi za Kamisheni Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 26	Uwezo wa Kamisheni Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 27	Uwajibikaji na Uwazi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 28	Ripoti ya Mwaka Pamoja na Marekebisho Yake.

Kifungu cha 29	Ripoti ya Mwaka Juu ya Hali ya Utumishi wa Umma Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 30	Kinga kwa Watoa Taarifa Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 31	Waziri wa Utumishi wa Umma Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 32	Uwajibikaji wa Waziri wa Mambo ya Utumishi wa Umma Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 33	Uwanzishwaji wa Tume za Utumishi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 34	Muundo na Sifa za Wajumbe Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 35	Muda wa Mjumbe Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 36	Kazi na Uwezo wa Tume ya Utumishi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 37	Uendeshaji na Mambo Mengine Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 38	Mamlaka ya Mawaziri Katika Utumishi wa Umma Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 39	Uwanzishwaji wa Kamati ya Makatibu Wakuu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 40	Kuanzishwa kwa Afisi ya Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 41	Majukumu ya Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 42	Uwezo wa Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 43	Kazi za Mkuu wa Idara Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 44	Kufanya Mapitio ya Kazi na Shughuli Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 45	Ripoti ya Utekelezaji Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 46	Kusimamia Nidhamu na Uwajibikaji Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 47	Uanzishwaji Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 48	Idara za Afisi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 49	Kazi za Afisi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 50	Wajibu wa Kamisheni Katika Uwanzishwaji wa Taasisi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 51	Kuanzishwa kwa Wizara Pamoja na Marekebisho Yake.

Kifungu cha 52	Uwanjaji na Uwanzishwaji Upya kwa Wizara Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 53	Muundo wa Taasisi na Afisi za Kikatiba na Wakala Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 54	Idara Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 55	Wakala na Utendaji Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 56	Mipango ya Rasilimali Watu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 57	Uteuzi na Uwajiri Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 58	Ufumo wa Uendeshaji Serikali Kitaalamu na Umahiri Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 59	Masharti ya Kuingia Katika Utumishi wa Umma Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 60	Aina za Mikataba ya Uwajiri Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 61	Maelezo na Masharti ya Uwajiri Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 62	Muundo wa Utumishi na Mpangilio wa Kutangulia Kazini Pamoja na Marekebisho Yake.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, jana nilipokuwa nikichangia Mswada huu nilimuomba Mhe. Waziri katika kifungu hiki cha 62(2) ambacho kinazungumzia Muundo wa Utumishi na Mpangilio wa Kutangulia Kazini ambapo Katibu Mkuu Kiongozi atatoa kila baada ya muda.

Orodha ya mpangilio kutangulia kazini Zanzibar na orodha ya mpangilio wa kutangulia kazini katika utumishi wa umma. Ambapo kifungu cha pili kimewaunganisha viongozi wa kisiasa. Sasa ningemuomba neno viongozi wa kisiasa liondoshwe katika kifungu kile. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mheshimiwa nakubali tuondoe.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Tuendelee Mheshimiwa.

Kifungu cha 62	Muundo wa Utumishi na Mpangilio wa Kutangulia Kazini Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 63	Uainishaji wa Madaraka Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 64	Kupandishwa Cheo Kifungu cha 62 Pamoja na Marekebisho Yake.

Kifungu cha 65	Kuhamisha Wafanyakazi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 66	Haki ya Kurudi Kazini kwa Mgombea wa Uchaguzi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 67	Maendeleo na Mafunzo kwa Wafanyakazi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 68	Kumalizika kwa Mkataba wa Ajira Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 69	Kuanzishwa kwa Vyeo vya Juu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 70	Sifa Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 71	Madhumuni na Maendeleo ya Huduma na Nafasi za Maafisa wa Kada za Watendaji Wakuu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 72	Wajibu na Kazi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 73	Maelezo ya Katibu Mkuu Kiongozi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 74	Kuachishwa kwa Kazi kwa Afisa wa Kada ya Utendaji Wakuu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 75	Mafaa Maalum na Vivutio Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 76	Vivutio vya Kustaafu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 77	Mazingira ya Kazi na Usalama Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 78	Afisi ya Usalama wa Serikali Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 79	Viwango vya Kazi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 80	Mahusiano Kazini Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 81	Kamati ya Nidhamu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 82	Mamlaka ya Kinidhamu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 83	Sababu ya Hatua za Kinidhamu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 84	Kusimamishwa Kazi kwa Afisa Aliye Chini ya Uchunguzi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 85	Utaratibu wa Masharti ya Kinidhamu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 86	Uwamuzi wa Mamlaka ya Kinidhamu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 87	Kuwepo kwa Adhabu za Kinidhamu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 88	Mapitio na Rufaa Pamoja na Marekebisho Yake.

Kifungu cha 89	Uwamuzi Dhidi ya Rufaa Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 90	Uwamuzi wa Dhidi ya Jambo Ambalo Haliwezi Kukataliwa Kukatiwa Rufaa Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 91	Kanuni Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 92	Kusitisha Uwamuzi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 93	Mfumo Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 94	Utekelezaji Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 95	Kumbukumbu za Utendaji Pamoja na Marekebisho Yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante nimesimama tena katika kuendelea kusaidia katika uwandishi vile vile. Katika marekebisho yaliyokuwa yamefanyika katika Kamati naomba kidogo kimejichanganya hichi cha 95 (1). Ili kisomeke kama kilivyokuwa kimepitishwa na kitafsirike sawa sawa ile tafsiri ya Kiingereza iliopo katika kifungu hiki.

Nilikuwa naomba na ndivyo ilivyokuwa makubaliano katika Kamati kwamba baada ya neno "**Afisi Kuu"** pale inapoanzia yale maneno itasimamia mstari ule mpaka neno mawasiliano mstari wa tatu yaondoke. Ili isomeke "**Afisi Kuu itakuwa na dhamana ya usimamizi"** halafu inaendelea mpaka mwisho. Kwa hivyo haya maneno kuanzia itasimamia mpaka neno mawasiliano lilokuwepo mstari wa tatu yaondoke ili sasa isomeke na maana kama iliyokusudiwa katika ile tafsiri ya kiingereza.

Kifungu cha (2) (c) mwisho wa ukurasa huo huo nilikuwa naomba tuweke sawa pale mstari wa pili. **Taasisi za Utumishi wa Umma zinatekeleza vigezo vya kwanza**, halafu **vya sheria**. Tuongeze pale **za nyaraka za taifa** kwa sababu hata ukisoma wa kiingereza. Sijui kama nafahamika Mwenyekiti.

Kifungu cha 95(2)(c) mwisho wa ukurasa wa 49 mstari wa pili kwamba taasisi za Utumishi wa Umma zinatekeleza vigezo vya sheria. Tuongezee za Nyaraka za Taifa. Kwa sababu ukisoma katika Kiingereza zinazungumzia sheria zinazo-*govern achieve* katika nchi, sio sheria tu kama ilivyowazi wazi. Kwa hivyo nilikuwa naomba marekebisho hayo mawili Mhe. Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mheshimiwa ni kweli, marekebisho kwenye Kamati yalikuwa yanasema hivyo lakini tulipokwenda kuchapa upya nafikiri hayakuingia. Kwa hiyo nakubaliana naye.

Kifungu cha 95 Kumbukumbu za Utendaji Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 96 Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Katika Utoaji Huduma katika Utumishi wa Umma Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 97 Kuanzishwa kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 98 Muundo wa Uwajibikaji Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 99 Jinsia Katika Utumishi wa Umma Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 100 H.I.V Ukimwi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 101 Ulemavu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 102 Motisha na Kukubalika Utendaji Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 103 Masharti ya Kanuni Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 104 Kufutwa kwa sheria Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 105 Masharti ya Mpito Pamoja na Marekebisho Yake.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza zima pamoja na mabadiliko yote na masahihisho yake)

(*Baraza lilirudia*)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawa Bora : Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima umepitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na mabadiliko yote na masahihisho yake. Sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali Mswada huo.

Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilikubaliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2011
Kusomwa kwa Mara ya Pili

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawa Bora: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2011 pamoja na marekebisho yake usomwe kwa mara ya pili.

Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilikubaliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mimi kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wajumbe wote kwa utulivu na mashirikiano makubwa ya kuendesha shughuli zetu. Tusiwe na hisia zozote kwamba labda Mswada huu tumechukua muda mkubwa. Ilikuwepo haja hiyo ya kufanya hivyo kwa sababu Mswada ni mkubwa ni muhimu. Bahati nzuri kwa mara ya kwanza tunaweka Mswada wa namna hii.

Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kuwa makini sana katika suala la kupitisha Mswada huu. Kazi kubwa hiyo ilianza kwenye Kamati, nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wake kwa kazi nzuri hiyo waliyoifanya. Yote hiyo ilikuwa na madhumuni ya kuufanya Mswada huu uwe bora na uwe ni mzuri. Mashirikiano siku zote ndiyo yanayofanya kazi ikawa ni nzuri zaidi. Sina budi niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kazi nzuri.

Mtakubaliana nami kutokana na kazi kubwa basi leo jioni tusije. Na kimsingi kazi kubwa ya shughuli yetu imemalizika isipokuwa ile iliyopangwa kwa ajili ya kesho. Kabla ya kuahirisha Kikao nimeombwa nitoe taarifa mbili kama ifuatavyo.

1) Kumekuwa na mmong'onyoko mkubwa wa maadili kwa hiyo wananchi wa Kijichi Paje, wameandaa Jitimai ya Kimataifa pale. Mhe. Mjumbe Asha Abdu Haji akishirikiana na Mhe. Jaku Hashim Ayub wameniomba nidotoe taarifa kwenu kwanza mnaalikwa kwenye Ijitimai hiyo ili tukaungamane na wana kijiji wenzetu wa Paje.
   Pia kuna matayarisho yale aliyoyaomba Mhe. Waziri ya Maji. Na vile vile kuna mchango ambao aliyekuwa tayari kutoa mchango huo aonane na Mhe. Asha Abdu Haji ili achukue mchango huo kuweza kufanikisha shughuli hiyo muhimu itakayofanyika kijijini Paje.

2) Nimeomba nitoe taarifa na tangazo kwenu kwamba ule uchaguzi wa wanamichezo utakuwa leo hii. Nimeomba utumike ukumbi huu ili kuweza kufanyia huo uchaguzi. Mimi nakubali kuchagua viongozi wana michezo, kwa hiyo wanamichezo wote tunaombwa tubaki kwa ajili ya uchaguzi huo.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana. Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa kuahirisha Kikao hiki hadi kesho tarehe 28 siku ya Ijumaa mwezi wa 01 mwaka wa huu, saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 7:30 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 28/01/2011 saa 3:00 asubuhi)